**9 FEBRUARI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI**

**Kikao cha Nane – Tarehe 9 Februari, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ajili ya maswali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali. Tutaanza na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi ya kuweza kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ilikuwa inatoa fomu namba 2C ambazo zipo chini ya Bima ya Afya na fomu hizo ni fomu ambazo mgonjwa huwa anaandikiwa dawa zile zinazokosa katika Hospitali zetu za Serikali au hospitali za watu binafsi na hivyo Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sasa utaratibu huo umesitishwa. Kusitisha utaratibu huo Mheshimiwa Waziri Mkuu, unapelekea zile *pharmacy* zote ambazo zilikuwa zinatoa huduma hiyo, ambazo zimeingia mkataba wa kisheria na Bima ya Afya kuweza kutotoa huduma hiyo na hivyo kupelekea hizo *pharmacy* kuelekea kufungwa na hivyo kupoteza ajira nyingi ambazo ni kiu cha Serikali kwa ajira hizo, lakini pia kuondoa uchumi wa mtu mmoja mmoja amabao unachangia pia pato la Taifa.

Je, Serikali haioni ni muda sasa muafaka kurejea utaratibu huo ili sasa wananchi waweze kupata dawa kwa uhakika, lakini pia na hizi ajira ambazo ni kiu ya Serikali zisipotee, lakini na kusaidia hawa watu ambao wamefungua *pharmacy* hizo kuwainua kiuchumi na wenyewe waendelee kuchangia katika Pato la Taifa? Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nasikiliza hapa kwa makini, nikawa nawaza ni kwa namna gani hili swali litakuwa la kisera kwa kanuni zetu sasa na ninyi mnamuona Naibu Waziri wa Afya anataka yeye ndio ajibu, kwa hiyo ni dhahiri swali hili linatakiwa kuja kama swali la msingi ili Wizara ya Afya iweze kupata nafasi ya kujibu. *(Makofi)*

Kwa muktadha huo nitamuita Mbunge anayefuata, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tumekuwa tukiona jitihada zako za kuzunguka nchi nzima kukagua miradi mbalimbali ya

maendeleo. Lakini katika ukaguzi huo umekuwa ukikuta miradi hiyo haitekelezwi vizuri kwa maana kunakuwepo na ubadhirifu, wizi na uzembe wa aina mbalimbali na hata ripoti ya *CAG* imekuwa ikitoa ubadhilifu huo na wizi mara kwa mara katika ripoti hiyo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, nini kauli ya Serikali kuhusu hali hii ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara. Ni mkakati upi wa makusudi na wa maalum ambao Serikali inachukua ili kuhakikisha kwamba wizi na ubadhirifu katika miradi ya umma haitokei kabla haijafanyika ili basi wananchi waweze ku…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lemburis, Mbunge wa Arumeru kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inao mfumo wa kufanya tathmini kwenye sekta mbalimbali ikiwemo na kufanya mapitio ya mwenendo wa matumizi ya fedha na mali za umma kwenye sekta hizo. *CAG* ni taasisi mojawapo ambayo inakwenda kuona mwenendo wa matumizi ya mali na fedha za umma kwenye sekta zote za Serikali na ikibidi pia hata sekta binafsi ambayo ina maslahi ya moja kwa moja kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba wanapofanya kazi hiyo wanabaini mapungufu na wakati mwingine mapungufu hayo wachache wanafanya kwa makusudi na *CAG* anachokifanya ni kuishauri Serikali namna bora ya kudhibiti hali hiyo kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli na mimi nilipata nafasi ya kufanya ziara kwenye Halmashauri zetu, taasisi mbalimbali za Serikali na ninapokwenda wakati mwingine nakwenda na taarifa ya *CAG* ambayo pia inashauri Serikali namna bora ya

kusimamia maeneo hayo na kuchukua hatua. Sasa namna gani nzuri ya kuendelea kusimamia.

Mheshimiwa Spika, kwanza tunatambua mchango mzuri wa taasisi hii ambao pia unatuainishia na kubainisha mapungufu hayo kwenye sekta zetu za Serikali na kazi yake ya kuishauri Serikali tunachukua ushauri huo na kuufanyia kazi, pale ambako tunauona ubadhirifu wa moja kwa moja tunachukua hatua na pale ambako anashauri namna ya kuboresha tunafanya hilo na sasa Serikali yetu imeandaa mfumo mzuri sana wa kufatilia sekta zetu kabla *CAG* hajafika.

Mheshimiwa Spika, ofisi yangu, Ofisi ya Waziri Mkuu, imeanzisha sasa Kitengo cha Ufatiliaji na Tathmini kwenye Sekta za Serikali ambazo zinabaini mapungufu hayo kabla *CAG* hajafika na kitengo hiki tumekiimarisha zaidi na kimeshaanza kazi. Sasa hivi kinapita kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, taasisi mbalimbali za Serikali ili kuona hali hiyo, kufanya tathmini, lakini pia kushauri pale ambapo kuna mapungufu kwenye sekta hiyo kabla *CAG* hajafika, lakini tunapokuta mapungufu tunaendelea kuchukua hatua.

Kwa hiyo, niendelee kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko makini kwenye hili, inafatilia na itaendelea kufatilia ili kuweza kudhibiti mali na fedha za Serikali, iwe ni kwa ajili ya mradi au kwa matumizi ya kwawaida kwenye ofisi yote haya ni majukumu ambayo Serikali inayafanya, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nini mpango wa Serikali wa kugawa, kuongeza au kupandisha hadhi maeneo ya kiutawala ambayo yamekidhi vigezo. Kwa mfano, kugawa mikoa mikubwa kama Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Morogoro au kupandisha hadhi Halmashauri ambazo zinatakiwa kuwa Majiji kama Halmashauri ya Manispaa ya Moshi?

**SPIKA:** Hili la Manispaa ya Moshi, nadhani na lenyewe liko mahsusi linahitaji lijibiwe na Wizara ya kisekta.

Mheshimiwa Zaytun Seif Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nyakati mbalimbali tumeona Serikali yetu ikitoa misamaha ya kodi kwenye bidhaa zile muhimu ili basi kupunguza gharama kwa wananchi wetu. Mwaka 2019 tuliona msamaha wa kodi kwenye taulo la kike, lakini bei ya soko haikupungua na mwaka 2021 tuliona msamaha wa kodi kwenye simu janja, lakini bei ya soko haikuweza kupungua.

Je, ni ipi mikakati ya Serikali kwenye kudhibiti bei ya soko, pale ambapo misamaha hii ya kodi inapotolewa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika naomba kujibu swali la Mheshimiwa Swai, Mbunge wa Arusha kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba Serikali inao mfumo wa kutoa misamaha ya kodi pale ambako inajiridhisha kwamba eneo hilo linaloombewa msamaha linaweza pia kupewa msamaha huo na hiyo inatakana pia na mtizamo wetu ndani ya Serikali kwamba kunaweza kuwa

kuna maslahi, maslahi hiyo inaweza kuwa ni pamoja na ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema la kupunguiza gharama ya bidhaa hiyo au ya huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, mfano hivi karibuni tumeona kupanda kwa bei ya mbolea nchini na Serikali ilipogundua kwamba gharama ya kununua mbolea ya shilingi 110,000 au zaidi ni kubwa na kwamba Watanzania hawawezi kumudu kununua na kwamba ili kuleta maslahi kwa Watanzania, Serikali ilitoa msamaha wa kodi, wakati mwingine pia na kutoa ruzuku na kuwezesha kupunguza gharama ya upatikanaji wa bidhaa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali inaendelea na utaratibu huu pale ambako inaona kuna bidhaa au huduma yenye maslahi na tunaweza tukaamua au mtu anayetoa huduma hiyo akaomba msamaha wa kodi na msamaha ukitolewa matarajio yetu ni kuona kuwa gharama hiyo inapungua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba maeneo yote haya ambayo yanapata ruzuku, yanapewa msamaha wa kodi, tunayasimamia kuwa na maslahi kwa watumiaji, kwa Watanzania kwa sababu unaposema unatoa msamaha wa kodi lile pengo la fedha lililokuwa linatakiwa kuuzwa awali na hii ya sasa baada ya msamaha linalipiwa pia na Serikali. Kwa hiyo, gharama inabaki pale lakini Serikali inatoa mchango wake inaweza kulipia kile cha ziada ili mtumiaji aweze kupata faida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea kuratibu hiyo na kusimamia maeneo yote ambayo tunatoa ruzuku, msamaha kuwa yanauzwa kwa bei ambayo tumekubaliana na sasa iuzwe baada ya kutoa msamaha.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwahakikishie Watanzania tutaendelea kufatilia maeneo yote amabayo tumetoa

msamaha, tutaendelea kufatilia maeneo yote tuliyotoa ruzuku ikiwemo na mbolea kama ambavyo Wizara ya Kilimo na kila kiongozi wa Serikali tunapofanya ziara kwenye Wilaya huko, tunaendelea kutoa misamaha hiyo ili kudhibiti mfumuko wa bei. Huo ndio utaratibu unatumiaka ndani ya Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuchukua maeneo ya wananchi kwa ajili ya miradi ya maendeleo pale ambapo Serikali haina eneo la kufanya miradi hiyo hasa hasa miradi kama ya shule, hospitali au kupanua maeneo ya jeshi au uwekezaji, na baada ya kuchukua maeneo hayo hufanyiwa tathmini ili watu waweze kulipwa fidia. Hata hivyo kumekuwa na tatizo la ucheleweshaji wa kulipa fidia na sehemu nyingine kuingia hata mambo yasiyokuwa ya uaminifu katika utekelezaji wa ulipaji wa fidia.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini msimamo wa Serikali katika jambo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ng’enda, Mbunge wa Manispaa ya Kigoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu wa Serikali wa kuchukua maeneo mbalimbali ya ardhi yetu, kwa ajili ya

miradi ya maendeleo pale ambapo tunaona tunahitaji kutekeleza mradi maalum kwa maslahi ya Watanzania na kwa hili naomba nianze kueleza umma wa Watanzania kuwa ardhi yetu hii ni ya umma na Mheshimiwa Rais, ndio mdhamini wa ardhi hii. Mheshimiwa Rais anaweza kuchukua ardhi popote kwa maslahi ya umma, kwa lengo la kutekeleza mradi ambao unaweza kusaidia jamii ya eneo hilo kuutumia vizuri. Lakini tunapochukua ardhi hiyo huwa tunafanya tathmini ili kulipa fidia ya mali iliyoko kwenye ardhi, inaweza kuwa labda nyumba au mazao, lazima yafanyiwe tathmini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli mara kadhaa Serikali tumekuwa tukichukua maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya miradi ya umma na tunapokuta kuna mali imewekezwa na mtanzania huwa tunalipa fidia.

Sasa suala la ucheleweshaji ni taratibu vigezo kama havijakidhi; moja, wakati tunafanya zoezi la tathmini ni lazima tufahamu nani hasa yuko hapo na amewekeza hiyo na lazima kuwe na viambata vinavyoeleza kwamba huyu ndio mwenye eneo hili na tunampiga na picha, thamani inatambulika hapo hapo na yeye anatambua thamani yake halafu maandalizi ya kulipa fidia yanafanywa.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji unakuja kama zoezi hilo halijakamilika au kuna migogoro ya wao kwa wao, wanagombania eneo hilo kwa umiliki, hapo inaweza kuchelewa, na wakati mwingine tathmini na idara inayolipa labda kama ilikuwa inategemea bajeti kunaweza kuwa na-*delay,* lakini niendelee kuwahakikishia Watanzania ambao wanafikiwa maeneo yao kwa ajili ya tathmini, kwa ajili ya kutumika kwa miradi na tunafanya tathmini kama kunachelewa. Hakuna Mtanzania, hakuna mwananchi ambaye anachukuliwa ardhi na huku akiwa amewekeza, tukafanya tathmini akakosa stahiki yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali itaendelea kusimamia maeneo hayo na kama yako maeneo labda pale Kigoma kuna eneo ambalo tathmini ilishafanyika na bado hatujalipa kutakuwa na moja kati ya haya niliyoyasema; au kuna migogoro, labda idara ilifanya tathmini hiyo na ilikuwa haijajiandaa na kama haijajiandaa tunarudi kwenye sheria yetu ile ya kwamba toka siku ya tathmini mpaka siku ya malipo ikiwa zaidi ya miezi sita lazima ifanyike tathmini tena ili kujua thamani halisi ya wakati huo ili sasa kuwezesha idara, lakini wananchi kujipanga kwa ajili ya kupata fidia yao.

Mheshimiwa Spika, hayo ndio maelezo sahihi ya Serikali ambayo yanatumika wakati wote tunaopohitaji kuchukua eneo na kufanya tathmini na kulipa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ulianzishwa kama namna mojawapo ya kutatua changamoto ya ajira kwa vijana na chanzo kikuu cha mapato katika mfuko huu ni bajeti inayotengwa na Serikali kupitia Bunge hili tukufu na kwa miaka saba mfululizo, mfuko huu umekuwa hautengewi fedha zozote. Mwaka 2022 mfuko huu umetengewa shilingi bilioni moja ambayo inatakiwa kwenda kwa vijana katika Halmashauri zote 185 nchi nzima. Fedha hizi ni ndogo, hazitoshi na hivyo hata *impact* ya mfuko huu haionekani kwa vijana. Sasa nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inatafuta vyanzo vingine vya mapato katika mfuko huu ili kuutunisha na kuuongezea tija zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu hili swali ni mahsusi, lakini kwa sababu lipo chini ya Wizara yako, unao uchaguzi kwa sababu yupo Waziri anayesimamia hilo jambo.*(Kicheko)*

Kwa hiyo, unao uchaguzi umkabidhi Waziri ampatie majibu Mbunge, kama unayo kwa sababu iko chini ya Wizara yako unaweza ukamjibu Mheshimiwa Mbunge.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu ridhaa yako nimjibu Mheshimiwa Ng'wasi na nataka nimjibu kwa sababu ameuliza swali ambalo liko ofisini kwangu na nalifahamu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inayo Wizara inashughulikia vijana na kwenye eneo hili, ziko programu mbalimbali za uwezeshaji kwa vijana wetu na tumeanzisha na mfuko huo wa vijana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kwa miaka 7 haujatengewa fedha, lakini katika kipindi hiki hiki tulishatenga fedha zaidi ya bilioni moja, kumbukumu zangu nilizonazo ofisini zinaonesha mwaka 2017 tulitenga bilioni moja, hazitoshi kwa mahitaji ya vijana nchini, tukaongeza tena bilioni nane, tukawa na bilioni 1.8 na tulishaanza kuzitoa. Tunatoa kwa vijana kwenye halmashauri zetu ambao wanakidhi vigezo na vigezo kukidhi vigezo ni moja kwanza ufahamike na Ofisi ya Halmashauri, uko wapi? Unafanya nini ili unapopata ile fedha, basi Ofisi ya Halmashauri ambayo inaratibu vijana iwe inafahamu huyu kijana yuko wapi na kwa kuwa sehemu kubwa inaweza kuwa ni mikopo au *support* lakini tujue kwamba kama ni mkopo unaweza kuurejesha.

Mheshimiwa Spika, sasa nini kinafanyika? Kwanza tumeunda mfuko maalum huu mfuko ambao tumeunda na tunao mwongozo wa kuendesha mfuko huo. Na mfuko huu, mbali ya Serikali lakini pia huwa tunatoa fursa kwa wadau kuuchangia na sasa tumeanza kuona taasisi mbalimbali

ambazo zinasaidia Serikali yetu katika kukuza uwezo wa vijana uweze ku-*support*.

Nini Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya, baada ya kuona kwamba kiwango hiki hakitoshi? Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu inalenga kuwawezesha vijana kumudu, kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi, sisi tumeanzisha programu ya uanangezi, programu ambayo inawachukua vijana na kuwapeleka kwenye vyuo mbalimbali nchini, ili kupata ujuzi ambao utamuwezesha yeye mwenyewe kujiajiri. Tunawapeleka *VETA*, tunawapeleka vyuo ufundi binafsi, lakini tunawapa pia mafunzo ya huduma, utoaji huduma, kuwapeleka mahotelini namna ya kutoa huduma kwenye hoteli mbalimbali na anapomaliza kozi yake ya miezi sita, ambayo inagharamiwa na Serikali anakuwa tayari anaweza kujiajiri au kuajiriwa na sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, programu hizi zipo nyingi na tunaendelea kuziratibu na nikuhakikishie najua Mheshimiwa Ng'wasi ni Mbunge na unawakilisha vijana tunao mpango wa kuhakikisha vijana hawa wanakuwa na uwezo, lakini wanakidhi vigezo vya kuweza kupata *support* kupitia mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, lakini hatujaishia hapo tu, Serikali tumeendelea pia kutoa maagizo kwa Halmashauri za Wilaya, ule mfuko unaokopesha wa asilimia nne, wenye kipengele cha vijana cha asilimia nne nao pia wananufaika, na sasa nishauri ili waweze kunufaika waunde vikundi kwenye maeneo yao. Mmoja mmoja ni ngumu, unaweza kukosa kufikia vigezo, lakini mkiwa kikundi inakuwa rahisi zaidi mtafanya shughuli ya pamoja. *(Makofi)*

Kwa hiyo mfuko wa halmashauri wa asilimia nne nayo inasaidia katika halmashauri zote katika kutambua vijana na kuwa-*support* ili waweze kufanya shughuli zao kwa lengo la kuongezea uchumi wao. Kwa hiyo, programu ya Ofisi ya

Waziri Mkuu, programu iliyoko Ofisi ya Rais, TAMISEMI hizi zote kwa pamoja, lakini pia michango tuliyopata kwa wadau yote hii inaimarisha katika kuwawezesha vijana kufikia katua na malengo waliyojiwekea, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni sera ya Serikali kuhakikisha kwamba inafikisha umeme vijijini kwa mpango wake wa *REA* na ni ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ilikuwa kwamba ikifika Desemba, 2022 vijiji vyote Tanzania Bara viwe vimepata umeme kupitia mpango huu, lakini kumekuwa na kusuasua kwa utekelezaji wa mpango huu, lakini pia muda umepita na vijiji vingi bado umeme huu haujafika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini mkakati wa Serikali wa muda mfupi kuhakikisha kwamba tunarudisha matumaini kwa Watanzania katika kutekeleza sera hii?

**SPIKA:** Hilo swali limeulizwa kwa mapana kwa maana ya sera, lakini kuna Wizara inayoshughulika na hili jambo, kwa hiyo nadhani tutoe nafasi swali hilo liulizwe kama swali la msingi na hivyo ili Wizara ipate nafasi ya kueleza mkakati wake.

Mheshimiwa Nusrat Shabani Hanje, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, malengo ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana mwaka 1993 ilikuwa ni kuhakikisha inawapatia mtaji vijana kwa mikopo ya masharti nafuu ili waweze kujikwamua kiuchumi, lakini kwa muda sasa mfuko huu umekuwa ukitengewa fedha, lakini vijana wanakosa hizo fedha kwa kiasi kwa sababu ya kukosa vigezo, lakini pia tunafahamu zipo halmashauri ambazo zinakosa asilimia 10 zile ambazo ni *four, four, two;* nne za vijana, nne za wanawake na mbili za walemavu, kwa sababu hazina mapato ya kutosha.

Ni kwa nini sasa Serikali isitumie Mfuko wa Maeneleo ya Vijana kama *equalization fund* kuziwezesha zile halmashauri amabzo zina mapato machache, mapato kidogo ili na zenyewe ziweze kutoa zile asilimia nne za halmashauri ili vijana waweze kupata mitaji kama ambavyo yalikuwa malengo ya kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo Vijana? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa Wabunge wanawakilisha vijana, naona maswali yao yote yanafanana. Naona swali lao linafanana lakini unaweza ukarejea pengine kwa ile sehemu ambayo amejaribu kutofautisha na swali la mwanzo kwa maana ya pesa zile zinazotengwa badala ya kwenda moja kwa moja kwa vijana kwenye zile halmashauri ambazo hazina uwezo, ndio zipelekewe hizo pesa. Pengine kipengele hicho ndio kinaonesha tofauti ya swali la mwanzo na hili. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hanje, Mbunge wa Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa majibu ya swali la awali linalohusu vijana kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuwawezesha vijana nchini kwa kuwatengea fedha kupitia mfuko, lakini pia kwa kutengeneza vigezo

ambavyo vinaweza vikakidhi kwa ajili ya vijana hawa waweze kunufaika na mfuko wao.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la kutunisha mfuko nimeeleza kwamba Serikali inajitahidi kila mwaka kutenga fedha kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. Tulitenga bilioni moja, tukaongeza milioni 800 na bado tutaenedelea kutenga, lakini bado hazitoshi na nimeeleza awali. Kwa kutotosha fedha hizi bado tunaendelea kuhusisha na Wizara nyingine zenye programu za vijana ikiwemo na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo imetenga mfuko na fedha kupitia mapato ya ndani asilimia 10; asilimia nne ni za vijana, lengo ni kutunisha ule mfuko.

Mheshimiwa Spika, sasa na tumefungua milango kwa taasisi binafsi ambazo na zenyewe zinashughulikia vijana na Serikali yetu tuna marafiki wengi ambao pia wanaona jitihada zetu za kuwawezesha vijana, nazo pia zinachangia na ndio kwa sababu tulianzisha mfuko ili kurahisisha pia michango yao kuingia pale, jukumu letu Serkali ni kuusimamia mfuko uweze kuleta manufaa.

Mhehimiwa Spika, lakini la pili hivyo vigezo ambao vijana wengi wanakosa vigezo, tunaposema kukosa vigezo ni pale ambako kijana anakuwa hana anwani maalum, kijana huyu ni mzaliwa wa pale Singida, lakini anakutwa yupo Dar es salaam; kule Dar es Salaam anahitaji pia kuwezeshwa ni lazima tujue huyu hapa Dar es salaam anakaa wapi? Mtaa gani anafahamika na viongozi wa mtaa huo?

Sasa sehemu kubwa ya vijana wetu wanashindwa kukidhi kigezo hicho kwa sababu na wenyewe wako *mobile,* wanatembea huku, wanaenda huku katika kutafuta manufaa hayo, katika kujiwezesha kiuchumi. Lakini nini tunakifanya sasa, tunaendelea kuwahamasisha vijana kwenye halmashauri zetu na tunawatambua vijana hawa kupitia Idara yetu ya Maendeleo ya Jamii kwenye

halmashauri, tunawatambua vijana kwenye vijiji, idadi yao, mahitaji yao ya shughuli za kiuchumi, huku Ofisi ya Waziri Mkuu kama nilivyosema tumeandaa mpango wa mafunzo ya vijana hawa ili kuwawezesha kuwa mafundi, kuwa na uwezo wa kufanya kazi mbalimbali na mafunzo haya yanachukua miezi sita, yanagharamiwa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, wanaenda vyuoni wakisoma miezi sita, wanarudi wanakuwa tayari wanakuwa na vigezo vya kupata mikopo kwa sababu tayari tunafahamu anakokaa, ana ujuzi, unajua akichukua fedha anaenda kuitumia kwa ajili ya moja, mbili, tatu. Jitihada hizi zinaendela kupanuliwa wigo ili sasa tuweze kuwafikia vijana wote.

Mheshimiwa Spika, na mwisho niliishia na ushauri kwa vijana wetu, pindi wanapomaliza mafunzo haya, wanapokuwa pamoja kwa maana ya kuunda vikundi wanakuwa vizuri zaidi, huo ni ushauri na wanapofikiwa ni rahisi wao wakiwa kikundi kukopesheka kuliko wakiwa mtu mmoja mmoja.

Kwa hiyo, tunaendelea kufanya maboresho kwenye maeneo yote haya; kwanza kuwa na vigezo, lakini mbili kuweza kuwafikia na kutunisha mfuko ili waweze kunufaika. Jitihada hizi zinaendelea na tunaendelea sasa kukusanya Wizara zote ambazo zinahusika na vijana ikuwemo na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu yenyewe na wadau ambao tunao na jumuiya mbalimbali za dini na vijana zote hizi zinatumika katika kuhakikisha tunakusanya nguvu ya pamoja kuwawezesha vijana ili kuweza kuwawezesha kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, huo ndio utaratibu tunautumia kwa sasa, lakini nikiri kwamba maswali yote mawili yanaweka msisitizo kwa vijana, kwa hiyo Serikali tutapanua wigo wa kutoa huduma kwa vijana zaidi ili malengo ya vijana yaweze kufikiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya kawaida, tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali sasa aulize swali lake.

Na. 122

**Vifaa tiba katika Hospitali Mpya ya Wilaya ya Mbarali**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya maboresho makubwa ya miundombinu katika sekta ya afya

ikiwemo ujenzi wa hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imepeleka vifaa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 418 kwa ajili ya jengo la huduma za dharura *(EMD)*, pamoja na mashine ya kisasa ya *X-ray* ya shilingi milioni 155 hospitali ya Wilaya ya Mbarali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 69.95 katika bajeti ya mwaka 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Mbarali ambayo imetengewa shilingi milioni 100, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtega, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na napongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa maboresho makubwa, hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, moja; ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha hasa madaktari na wauguzi?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili; ni lini Serikali itapeleka vifaa vya kutosha katika Kituo cha Afya Chimara lakini pia Kituo cha Afya Igurusi ili waweze kutoa huduma za upasuaji? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshapeleka vifaa tiba vya shilingi milioni 418 katika Halmshauri ya Mbarali, lakini katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 69.65 kwa ajili ya kupeleka vifaa tiba kwenye vituo vya afya na hospitali za halmashauri pamoja na zahanati zilizokamilika. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi la kupeleka vifaa tiba kwenye vituo vyetu ni endelevu, lakini pia vituo hivi vya Mbarali vitapata vifaa tiba hivyo.

Mheshimiwa spika, lakini pili katika mwaka wa fedha uliopita Serikali iliajiri watumishi 10,462 na Halmashauri ya Mbarali ilipata watumishi 51 wakiwemo madaktari na wauguzi na Seriakli itaendelea kupeleka watumishi hao katika halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mapera kilichopo Mbinga Vijijini hakina vifaa tiba vya msingi ikiwemo *ultrasound*, *x-ray* na hamna *generator* hali inayozorotesha upasuaji hasa nyakati za usiku. Fedha ambazo Serikali imetenga, je, na Kituo cha Afya cha Mapera kimetengewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Judith Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kituo hiki cha afya cha Mapera kilichopo katika Halmashauri ya Mbinga ni moja ya vituo ambavyo vimeingia kwenye orodha ya kupelekewa vifaa tiba katika bajeti ya mwaka wa fedha huu 2022/2023, lakini pia tutaendelea kutenga katika bajeti ijayo ya 2023/2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba mfano *x-ray machine* na *ultrasound* kwenye Vituo vya Afya vya Kamsamba, Mkulwe, Msangano, Ndalambo pamoja na Kapere?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Jimbo la Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu na sera za afya, vituo vya afya vinapelekewa mashine za *ultrasound* lakini vituo vya afya ambavyo vinapata mashine za *x-ray* ni baada ya tathmini ya kuona idadi ya wananchi wanaotibiwa katika maeneo hyo.

Kwa hiyo, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge, tufanye tathmni ya kuona idadi ya wananchi wanaotibiwa kaita Kituo cha Kamsamba na vingine ambavyo amevitaja kama vinakidhi sifa za kuwa na mashine za *x-ray,* lakini nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa

Halmashauri ya Momba kwamba mashine za *ultrasound* ziko ndani ya uwezo wa halmashauri kununua wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kuongeza nguvu katika maeneo hayo, ahsnate.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kumekuwa na mkanganyiko kwa hizo pesa zilizopelekwa katika halmashauri kwa sababu wengine hawajui kama ziende kwenye vituo vya afya au kwenye zahanati.

Sasa Serikali haioni sababu ya kuweka maelekezo maalum kabisa kwamba hizi pesa *either* ziende kwenye kituo cha afya na hizi ziende kwenye zahanati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela, Mbunge wa Jimbo la Lulindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inapopeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati au vituo vya afya au hospitali za halmashauri inapeleka na barua ya maelekezo kwa Mkurugenzi kwamba fedha zilizoletwa ni kwa ajili ya kujenga kituo cha afya eneo gani au zahanati eneo gani au hospitali ya halmashauri eneo gani?

Kwa hiyo, naomba nirudie kusisitiza kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kwamba wazingatie maelekezo yanayotolea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI mara fedha zinapopelekwa katika ujenzi wa vituo hivi, ili kuepuka mkanganyiko ambao Mhehimiwa Mbunge ameusema, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa.

Kituo cha afya cha Umbwe ambacho ni ndio kituo pekee cha afya katika Tarafa ya Kibosho hakina gari la kubeba wagonjwa; je, Serikali ina mpango gani wa kutupatia gari la kubeba wagonjwa katika kituo hiki?

**SPIKA:** Mheshimwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimia Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Umbwe ni kituo pekee katika tarafa hiyo na kinahudumia wananchi wengi na hakina gari la wagonjwa. Mheshimiwa Ndakidemi amekuwa akifuatilia mara kwa mara, lakini naomba nikujulishe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mwaka huu wa fedha tutapeleka magari ya wagonjwa katika halmashauri zote 184, lakini pia tutapeleka magari ya huduma za afya kwa maana usimamizi katika halmashauri zote 184, ikiwemo Halmashauri hii ya Moshi Vijijini, na hivyo ni maamuzi ya halmashauri kuona inakipa kipaumbele kituo hiki cha afya cha Umbwe ili kiweze kupata gari hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante; je, ni lini Serikali hii itapeleka vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Bashnet na Madunga katika Jimbo la Babati Vijijini ambavyo viko tayari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kituo hiki cha Afya cha Bashnet, lakini na vituo vingine vya afya ambavyo vimekamilika katika Jimbo la Babati Vijijini Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 69.95 katika mwaka huu wa fedha na tayari vifaa tiba vimeanza kupelekwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatoa kipaumbele pia katika kituo hiki cha afya ili kiweze kupata vifaa tiba hivyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naishukuru Serikali kwa kutujengea vituo vya afya ndani ya Jimbo la Hai.

Swali langu, ni lini sasa Serikali itatuletea vifaa tiba kwenye Vituo vya Afya vya Kwansira, Chemka na pale Kisiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba Kituo cha Afya cha Kwansira ambako mimi na yeye tulifanya ziara na kazi ya ujenzi iko hatua za mwisho, ni sehemu ya vituo ambavyo vinahitaji vifaa tiba mara baada ya kukamilika, lakini pamoja na hivi vituo vya afya vingine ambavyo amevitaja. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutenga fedha na kupeleka vifaa tiba kwenye vituo hivyo alivyovitaja ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi wa Hai, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Protas, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS**: Mheshimiwa Spika, ahsante, Kituo cha Afya cha Igalula katika bajeti tulikitengea milioni 450 na tumekwisha pokea milioni 450 lakini cha ajabu TAMISEMI mmeleta barua ya kugawa zile fedha kwenye vituo vitatu.

Je, kwa nini Serikali isione haja ya kukimaliza kabisa Kituo cha Afya cha Igalula katika vifaa tiba na kiendelee kutoa huduma stahiki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba arudie swali sijamsikia vizuri.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ya Serikali tulitenga shilingi milioni 450 katika Kituo cha Afya cha Igalula na Serikali imekwisha leta shilingi milioni 450 katika Kituo cha Afya cha Igalula. TAMISEMI mkaleta barua ya fedha zile zigawie katika vituo vitatu maana ya kwamba kila kituo kipelekewe shilingi milioni 150.

Je, Serikali haioni haja ya kumaliza matatizo ya Kituo cha Afya cha Igalula kuliko kuzigawa hizi fedha na kituo kile kiendelee kutoa huduma stahiki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venant David Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapopeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwanza dhamira ya kwanza ni kuhakikisha kwamba vituo vile vinakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi mara moja.

Naomba sasa niichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imepeleka shilingi milioni 450 lakini kuna maelekezo ya kuzigawa fedha hizo katika vituo vitatu, nikitoka hapa nikaa na Mheshimiwa Mbunge lakini nifuatilie kuona sababu za msingi za kufanya hivyo na kama hakuna sababu tutakubaliana tukamilishe Kituo cha Afya cha Igalula na hatimaye tuendelee na vituo vingine kwa mujibu wa utaratibu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Jenista kwa kazi nzuri anayoifanya katika kile kijiji kwenye zahanati.

Je, ni lini sasa Serikali mtapeleka vifaa tiba kwenye Zahanati ya Mdunduwaro ili ianze kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ntara lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa namna ambavyo wameendelea kusimamia ujenzi wa Zahanati ya Mdunduwaro na ni kweli kwamba Mheshimiwa Jenista Mhagama amekuwa akilifuatilia na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara amekuwa akilifuatilia.

Nimhakikishie kwamba tulishakubaliana kwamba kwanza Zahanati ile ikamilike kabla ya tarehe 30 Machi, isajiliwe, lakini tumeshakubaliana vifaa tiba vitapatikana ndani ya halmashauri kwa sababu tayari wana vifaa ambavyo havitumiki katika vituo vingine, lakini na Serikali itaongezea kuhakikisha kwamba kinaanza kutoa huduma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali.

Kituo cha Afya cha Upugi kilikarabatiwa kwa hali ya juu sana na kuletewa mitambo ya kisasa, lakini hela zilipungua kwa kujengea jengo la mashine ya *x-ray* na *ultrasound*. Huu mwaka wa nne zile mashine hazijafunga.

Je, lini Serikali itajenga jengo la kuweka mashine ya *x-ray* na *ultrasound* katika Kituo cha Upugi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Almas Maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ikipeleka fedha katika ujenzi wa miundombinu ya huduma za afya, kwanza tunapeleka kwa awamu. Awamu ya kwanza, majengo ya *OPD*, majengo ya maabara ya mama na mtoto; lakini awamu ya pili tunatenga majengo mengine ya Vipimo ya *x-ray*, *ultrasound* na wodi, lakini kwa taarifa ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitoa kwamba fedha hazikutosha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya *x-ray* na *ultrasound*, nimhakikishie kwamba Serikali kwa maana ya fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri na Serikali Kuu tutakaa tuone wapi tunapata fedha ili tuweze kukamilisha majengo hayo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Nakapanya, jengo la upasuaji limekamilika na baadhi ya vifaa vya upasuaji vipo na *ambulance* ipo.

Je, ni lini Serikali itakamilisha baadhi ya vifaa vya upasuaji ili kituo kile kianze kutoa huduma ya upasuaji na kumsaidia mama na mtoto katika kituo kile? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya hiki cha Nakapanya ni kweli kwamba kuna baadhi ya vifaa tiba vimeshafika, lakini tayari tumepanga watumishi kwa ajili ya kuanza kutoa huduma na tunafahamu kwamba kuna baadhi ya vifaa tiba hasa kwenye jengo la upasuaji bado havijafika.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye bajeti ya mwaka huu, vituo vyote hivi vya afya vilivyokamilika ikiwemo hiki cha Nakapanya kimetengewa fedha kati ya ile shilingi bilioni 69.95 kwa ajili ya kupeleka vifaa tiba ili vianze kutoa huduma za upasuaji kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi, sasa aulize swali lake.

Na. 123

**Kuboresha Uwanja wa Mpira wa Boma Masasi Mjini**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itauboresha uwanja wa mpira wa Boma uliopo Masasi Mjini kwa kiwango kinachofaa kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana wa Masasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Taifa ya mwaka 1995 kifungu cha 7(i) hadi (vii), jukumu la ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya michezo ni jukumu la Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na wadau wa sekta ya michezo zikiwemo taasisi, mashirika na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, hivyo, napenda nitoe rai kwa Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Mji Masasi kuzingatia matakwa ya sera ya michezo kwa kutenga fedha kutoka katika mapato ya ndani kwa ajili ya kujenga na kukarabati miundombinu ya michezo kwenye maeneo yao kama zilivyofanya Halmashauri za Ruangwa, Geita, Nyamagana, Bukoba na Babati Mjini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. GEOFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa tunashida kubwa ya ajira kwa vijana, lakini pia kwa kuwa tunajua kuna vipaji vingi vya vijana kwenye nchi yetu, lakini pia kwa kuwa tunafahamu ziko nchi zimewekeza vya kutosha kwenye vijana kama vile Brazil, Congo DRC, Senegal, Nigeria, Ghana, naomba sasa niulize maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ningependa kujua kwamba kutokana na umuhimu huu ambao nimeusema, Wizara inaweza ikatengeneza utaratibu kwa kuanza kuweka bajeti kidogo ya kuweza kusaidia Halmashauri za Miji Midogo

ambayo haina uwezo wa kibajeti kuweza kuendeleza viwanja ambavyo tayari vipo kwenye maeneo yale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunafahamu kwamba kuna juhudi kubwa zinafanywa na watu binafsi kwenye kuendeleza vijana kupitia shule mbalimbali za soka…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe, sehemu ya kwanza umeshatoa maelezo, kwa hiyo, maswali yako nenda moja kwa moja, sasa.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ndio; je, Serikali inaona ni muhimu sasa kuweza kusaidia vituo vya kulelea vijana na hasa ukuzaji wa vipaji vya soka na michezo mingine ili tuweze kupata vijana ambao wameandaliwa vizuri kwa ajili ya timu ya Taifa na kuweza kupata ajira nje ya nchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwambe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza alipenda kufahamu kama Serikali tupo tayari ku-*support* halmashauri ambazo bajeti zao ni chache na wasingeweza kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya msingi nimesema kwamba jukumu hili ni la Serikali Kuu, lakini pia Serikali za mitaa. Naomba nipongeze Halmashauri ya Masasi wao wameshaanza kuzungusha uzio katika uwanja ule, lakini pia sisi kwa upande wa Wizara pia tumeanza kujenga baadhi ya viwanja na katika mwaka huu wa bajeti, tulitenga viwanja

zaidi ya saba. Pale bajeti ambapo itaruhusu sisi tutaendelea ku-*support*.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili alitaka kufahamu ni kwa kiasi gani tunaweza tuka-*support* vituo vya kukuza vipaji *(academies)*.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tunaandaa mazingira wezeshi kuhakikisha hizi *academy* zinafanya vizuri na mpaka sasa tuna *academies* binafsi zaidi ya 84. Kwa hiyo, sisi Wizara tutaendelea ku-*support*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kuna watu mna kelele hata sielewi, kama niwasimamishe ama nifanyaje, maana kila mtu akigonga kwenye Bunge hili tutasikilizana kweli? Hatutasikilizana, kwa sababu nawaona Wabunge wengi mmesimama na kila mtu anagonga. Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la msingi.

Kwa kuwa shule nyingi sana za sekondari, za msingi na vyuo zina viwanja vibovu sana na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna baadhi ya halmashauri tayari zimeanza kutenga hizo fedha…

**SPIKA:** Swali, swali, swali.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hilo kwa sababu watoto wetu wanakosa haki yao ya msingi ya kutengeneza vipaji vyao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara na kama Serikali tulishatoa kauli kwamba katika shule zetu tuhakikishe tuna miundombinu ya michezo. Hivyo nitoe rai kwa halmashauri zetu, vyuo na maeneo ambako vijana wetu wanahitaji miundombinu hiyo waendelee kutenga, lakini wavitunze na waviendeleze.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, wakati Naibu Waziri anajibu maswali yake anaonesha jukumu kuu la Serikali pamoja na Serikali za Mitaa ni kujenga, kuhakikisha kwamba viwanja vinajengwa, lakini kuna halmashauri ambazo kwa mwaka mapato ya ndani hayafiki hata shilingi bilioni moja. Hapo ametutajia mfano Halmashauri ya Geita ambayo inapata mrabaha tu shilingi bilioni sita, hao wana uwezo wa kujenga.

Ninataka nijue, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha zile halmashauri ambazo hazina uwezo zinajengewa viwanja walau vyenye hadhi ya kuhodhi ligi ya mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru, naomba nijibu swali moja la Mheshimiwa Esther, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba suala la michezo ni hitaji la wananchi wetu na tunafahamu kwamba vipaumbele vyetu katika nchi ni pamoja na kuhakikisha magonjwa yasiyoambukiza yanaweza kupigwa vita na wananchi wanakuwa salama. Pamoja na kwamba bajeti

zetu hazitoshi katika halmashauri, nitoe rai kwa halmashauri zote kutenga fedha hizi kwa kuwa tusipotenga fedha hizi maana yake hatutekelezi sera hii ya maendeleo ya michezo.

Kwa hiyo, hata kama bajeti zetu ni ndogo tutenge, kwa mfano Halmashauri hii ya Masasi, Mheshimiwa Mbunge pia ametenga sehemu ya Mfuko wa Jimbo kuhakikisha ana-*support* jitihada za halmashauri, kwa hiyo, tuendelee kutenga fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi ni moja kati ya viwanja kongwe nchini ambacho kiko katika Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha uwanja huo ili na wenyewe uweze kutumika katika michezo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu pia tunapojenga viwanja hivi tunaangalia na ukanda, lakini pia katika jitihada za Serikali tumehakikisha kwenye vile vipaumbele vyetu kwa upande wa *academies* tulizozianza, Tabora tulianza nao.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Hawa naomba nipokee ombi hili kwamba tutaendelea kutenga fedha kama ambavyo tumetenga kwenye viwanja saba vya mwaka huu, zaidi ya shilingi bilioni 10 tumeanza kazi, kwa hiyo tutawafikia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 124

**Fursa za biashara na uwekezaji Kimataifa**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuainisha nchi ambazo fursa za biashara na uwekezaji zinaweza kuiletea nchi yetu mapato na kupandisha pato la Taifa zinapatikana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza dhana ya diplomasia ya uchumi ambayo pamoja na mambo mengine ni kukuza biashara na uwekezaji toka nchi mbalimbali. Dhana hii inahusisha Sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na Balozi zetu imeendelea kutangaza fursa za kibiashara na uwekezaji zenye manufaa kwa Taifa letu. Ili

kuzitumia fursa hizi kwa tija zaidi, Wizara imeendelea na maandalizi ya Mpango wa Kitaifa wa kutekeleza Diplomasia ya Uchumi. Mpango huo utajumuisha sekta zote husika ikiwa ni pamoja na kuainisha maeneo muhimu ya kisekta yatakayochangia katika kukuza uchumi na Pato la Taifa. Mpango huu utajumuisha pia sekta binafsi na unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Desemba, 2023.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ya diplomasia ya uchumi kwa wananchi ambao ndiyo wadau wakubwa wa dhana hii ikilinganishwa na sasa inafahamika Kitaifa zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tumeona vyombo vingi vya habari na waandishi wa habari wakiwa nje ya nchi wakiripoti matukio hasi tofauti na fursa zilizoko Tanzania na zinazopatikana nje.

Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha waandishi wa habari walioko nje ya nchi wanatangaza nchi yetu na fursa zilizopo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza katika kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje ambayo imeweka msisitizo zaidi katika dhana ya diplomasia ya uchumi, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wananchi katika kuelezea fursa mbalimbali zinazopatikana nje ya nchi kupitia makongamano na vyombo vya habari, lakini pia na mitandao ya kijamii. Pia katika maonesho mbalimbali Wizara imekuwa ikitoa hiyo elimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, Wizara yetu au Serikali inachukua mkakati gani kwa ujumla kwa waandishi wa habari ambao wanapotosha hizi habari nje ya nchi. Kwanza ni kwamba balozi zetu zimekuwa *very active* mara zinapotokea taarifa hasi, basi mara moja wanashirikiana na vyombo vya habari vya nje katika kuhakikisha kwamba habari zinazotolewa ni za uhakika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza. Ahaa, Mheshimiwa Waziri amesimama.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba tu niongezee kidogo kwamba kuhusu mkakati wa kutoa elimu ya diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu jana wakati Kamati yetu ikitoa taarifa na kama ilivyoelekezwa pia na Kamati, tulieleza kwamba tunaandaa mpango mkakati wa kitaifa wa kutekeleza diplomasia ya uchumi na katika mpango huo, moja ya kitu kitakachojumuishwa ni mpango wa kutoa elimu kwa umma. Kwa hiyo, tutatumia mbinu mbalimbali kuboresha utoaji wa elimu ya umma pamoja na yale tunayoyafanya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili ambalo ni kuhusu tunafanya nini kushirikisha hivi vyombo vinavyotoa elimu hasi kuhusu Tanzania. Tunalifahamu hilo pamoja na hayo yanayofanyika, tayari tumeanza mazungumzo na vile vyombo vya nje hususani vile vinavyoongea Kiswahili kwa sababu sasa hivi tunakuza pia Kiswahili kuwaomba pia wadau wetu.

Mheshimiwa Spika, juzi nimekutana na Idhaa ya Kiswahili ya Uturuki ambao wamefungua idhaa ya kiswahili na moja ya kitu nilichowaomba na mtaona ni kwamba sasa watusaidie kutoa elimu chanya na taarifa chanya kuhusu Taifa letu hususan vivutio tulivyonavyo, fursa tulizonazo na waachane na kutoa elimu hasi. Wao wamekubali kwamba watatusaidia kushirikiana na idhaa nyingine, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ili kukuza uchumi biashara na uwekezaji katika mikoa ya Kusini, Lindi, Mtwara na Ruvuma, utekelezaji wa Mradi wa *Mtwara Corridor* ni muhimu sana.

Naomba kujua, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa mradi huo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Huu mradi upo chini yenu au upo chini ya Maliasili na Utalii? Mheshimiwa Tunza Malapo, huu mradi unaosema uko chini ya Wizara gani? Washa kisemeo, ehee uko chini ya Wizara gani?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, huo mradi kwa kweli una-*integration* ya Wizara nyingi kwa sababu hapo kuna ujenzi wa miundombinu, hapo kuna kutoa elimu, hapo kuna hawa watu wa mambo ya nje na namna wanavyo-

*interact* na Zambia, Msumbiji na wapi katika kukuza. Kwa hiyo, mimi nimeuliza hapo kwa sababu tunazungumzia biashara, uwekezaji pamoja na uchumi.

**SPIKA:** Sawa swali lako litajibiwa kama swali la msingi na Wizara inayohusika. Kwa hiyo ikishapelekwa Serikalini wao wataangalia ni Wizara gani inapaswa kujibu hilo swali.

Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 125

**Mradi wa Maji wa Kata ya Kihurio**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga mradi mpya wa maji safi na salama kuliko kuendelea na ukarabati wa Mradi wa Kata ya Kihurio ambao ulijengwa mwaka 1967?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango, Mbunge wa Same Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kujenga mradi mkubwa utakaoondoa kabisa tatizo la maji katika Kata ya Kihurio ambapo kwa sasa usanifu unaendelea na ujenzi utafanyika katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Aidha, katika kupunguza kero ya uhaba wa maji, Serikali kushirikiana na Jumuiya ya Watumiaji Maji inaendelea

kufanya ukarabati mdogo wa miundombinu ya maji kwenye Kata ya Kihurio. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikiri kwamba nimelipenda sana jibu la Serikali, lakini zaidi ya hapo naomba niulize swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa ni miaka 55 iliyopita tangu mradi huu ambao tunautumia sasa ulipojengwa na kwa kuwa walipoujenga mradi huu, chanzo cha maji kilikuwa kimoja kwa sababu Kata ya Kihurio ilikuwa na vijiji viwili tu na kwa kuwa sasa hivi Kata ya Kihurio ina vijiji vitano na *population* imekuwa kubwa sana takribani watu zaidi ya 10,000.

Je, Serikali haioni kwamba itakapojenga mradi huu mpya, ijenge vyanzo vya maji ambavyo ni zaidi ya chanzo kimoja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kuridhika na majibu ya Serikali, lakini vilevile nikupongeze kwa ufuatiliaji wa eneo hili la Kihurio.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara kila ongezeko linapotokea la watumia maji, tunaboresha vyanzo na *intake* zetu hivyo Mheshimiwa Mbunge hili nimelipokea na tutalizingatia wakati tunatekeleza mradi huu mkubwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Kwanza niishukuru Serikali kwa kuchimba maji katika Mradi wa Dambia na yanapatikana kwa wingi.

**SPIKA:** Swali?

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri lini mnajenga Mradi ule wa Dambia ambao unaufahamu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Massay kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeshachimba kinachofuata sasa ni hatua za usambazaji. Mradi huo ulioutaja ujenzi wake mara tukipata fedha tunakuja kuanza mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua mpango wa Serikali kutumia chanzo cha maji ya Ziwa Nyasa kuhudumia wananchi wa Kata ya Ruhuhu na Manda kwa sababu wananchi hawa wanaliwa sana na mamba hasa Kitongoji cha Panton?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kamonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Ziwa Nyasa kama chanzo endelevu tayari tuna miradi ambayo tumeanza kuitekeleza ukanda wa Nyasa pamoja na Ruhuhu. Tunafahamu eneo ambalo wananchi walikuwa wakiliwa na mamba na tayari tulishaagiza *RM* Njombe ameanza usanifu na anakuja kutekeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuiuliza Serikali; je, ni lini italeta mradi wa maji kwenye Tarafa ya Ngerengere?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Taletale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ngerengere ipo kwenye mpango wa Wizara, Mheshimiwa Waziri alishapita maeneo hayo. Mheshimiwa Mbunge tuko mbioni kuleta mradi huu wa maji tutatumia Mradi wa Chalinze ama Morong'anya kuhakikisha maji yanafika Ngerengere.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya 85% ya wakazi wa Wilaya ya Muleba hawana maji safi na salama; je, ni lini Serikali itaanza

ujenzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Wilaya ya Muleba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar, Mbunge wa Muleba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi ule wa mradi kutoka Ziwa Victoria upo kwenye mpango wa Wizara. Mara tutakapopata fedha tutaendelea kuzileta kwa mafungu ili mradi huu tuanze kuutekeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Ni lini Serikali itatekeleza maelekezo ya Waziri Mkuu ya kupeleka maji Kijiji cha Mtunduwalo iliyothibitishwa kwamba maji yale sasa hayawezi kutumika kwa matumizi ya binadamu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba arudie kijiji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya jina la kijiji?

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ni Kijiji cha Mtunduwalo, Kata ya Ruanda yanakochimbwa makaa ya mawe, maji yalikuwepo lakini sasa yamethibitika....

**SPIKA:** Ahsante, alitaka jina la kijiji, kwingine kote kaelewa, anataka jina la Kijiji basi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya viongozi wakuu yote tunayatekeleza na suala hili la kupeleka maji Ruanda nalo pia lipo kwenye utaratibu wa kuona kwamba hivi punde tunakuja kuhakikisha maji Ruanda yanaletwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante; swali langu ni je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maji kwenye Kata za Mwika Kaskazini, Mamba Kaskazini, Marangu Mashariki, Mwika Kusini na Kilemu kwa sababu miradi hiyo ina matatizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, sijamuelewa.

**SPIKA:** Ameuliza maeneo mengi, anataka kujua lini yatapata maji, lakini kwenye jimbo lake la Vunjo, kataja kata kama tatu hivi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kimei, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge, maeneo hayo yote uliyoyataja tuna miradi ambayo inaendelea na usanifu na miradi ambayo tunaitafutia fedha na katika mgao ujao na hata Jimbo la Vunjo nalo litakuja kupatiwa fedha ili miradi hii ianze kutekelezwa kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kujua ni lini mradi mkubwa wa maji kutoka Wilaya ya Ileje, Mto Songwe kwenda Jimbo la Tunduma utaanza kutekelezwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni mradi mkubwa na tayari umeshaanza utekelezaji kwa hatua za awali na tunatarajia maji Tunduma yatafika kwa sababu ni mradi ambao unajengwa kwa awamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela sasa aulize swali lake.

Na. 126

**Uhaba wa Maji -Jimbo la Kwela**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji kwenye Mji Mdogo wa Laela na Mpui katika Jimbo la Kwela?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji Mdogo wa Laela ni 51%. Ili kuboresha huduma ya maji Laela kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imeendelea na upanuzi wa Mradi wa Maji wa Laela na kazi zinazofanyika ni pamoja na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilometa 2.6 na ukarabati wa tenki lenye ujazo wa lita 225,000.

Aidha, kwa upande wa Kata ya Mpui yenye vijiji vya Mpui A na Mpui B wananchi wanapata maji kupitia chanzo cha mserereko na kisima na hali ya huduma ya maji ni 36%. Ili kupunguza kero ya maji Kata ya Mpui katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itachimba kisima kirefu kimoja.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu wa kumaliza tatizo la maji katika Mji Mdogo wa Laela na Kata ya Mpui, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itajenga mradi mkumbwa utakaotumia chanzo cha Ziwa Tanganyika au Mto Momba. Kwa sasa usanifu wa mradi huo unaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Clement Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya maswali madogo ya nyongeza.

Swali langu la kwanza, kwanza niipongeze Serikali kwa nia ya dhati ya kutatua kero kwenye Mji wa Mpui na Laela kwa kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika na Mto Momba.

Je, ni lini mkandarasi anayefnaya Mradi wa *Kaoze Group* ataripoti kuanza kazi kwenye Kata ya Kaoze, *Kilanga One* na Kipeta?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa tatizo la maji kwenye Mji Mdogo wa Mpui ni kubwa sana na mmesema mnaenda kuchimba kisima kimoja.

Je, Serikali hamuoni kuna haja ya kuendeleza mpango wenu wa kutumia Mto Kazila kupeleka maji katika Mji Mdogo wa Mpui?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deus Sangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimepokea pongezi, nikupongeze nawe pia kwa sababu ufuatiliaji wako katika suala hili umekuwa ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, lini mkandarasi atakwenda, ni mwezi wa tatu mwanzoni; wiki ya kwanza ya mwezi wa tatu tunatarajia mkandarasi huyu atafika *site* na kuanza kazi ya mradi.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Mto Kazila, ni kweli usanifu ulifanyika. Mto huu upo mbali kodogo wa kilometa 21 na ipo kwenye Wilaya tofauti na ambapo mradi upo. Kwa hiyo, tutachimba kisima kwa sababu tuna uhakika tutapata maji ya kutosha kama tulivyochimba maeneo mengine katika jimbo lako Mheshimiwa Mbunge. Itakapobidi kutumia Mto Kazila kwa sababu Wizara tunahitaji kuona tunatumia vyanzo vyote ambavyo vinatuletea miradi endelevu, Mto Kazila pia tutautumia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tatizo la upatikanaji wa maji katika Mji wa Muheza bado ni kubwa pamoja na juhudi nyingi zinazofanywa na Serikali.

Je, ni lini mradi wa miji 28 ambao tunaamini kwamba ndiyo suluhisho la kudumu la tatizo hili utaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamis, Mbunge wa Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa Miji 28; miradi hii yote imeshaanza kutekelezwa kwa hatua za awali za kukusanya taarifa na kukamilisha taratibu za kuanza ujenzi tayari zimeshaanza ni vile hamzioni wanakusanya taarifa. Mradi huu ni *design and build,* kwa hiyo mwezi huu wa tatu tunatarajia wakandarasi waanze kuonekana sasa *site* na kuanza kufanya ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Kigoma Mjini wameahidiwa mradi mkubwa wa maji kukamilika tangu mwaka 2020 na sasa tuko mwaka 2023 na mradi haujakamilika.

Je, ni nini kauli ya Serikali kwa wananchi wa Kigoma Mjini kuhusu mradi huo mkubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sylvia, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi Kigoma Mjini, mimi mwenyewe nimefika mwezi Novemba, mradi upo kwenye hatua za mwisho kabisa na maji yataanza kutoka hivi punde.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilwa, katika Vijiji vya Marendego na Kinjumbi kumekuwa na miradi ya maji ambayo imekuwa ikitekelezwa kwa zaidi ya miaka mitatu hivi sasa.

Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba ni lini miradi hii itakamilika ili wananchi wa vijiji hivyo waweze kupata huduma ya maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis, Mbunge wa Kilwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji hivyo ulivyovitaja Mheshimiwa Mbunge ni kweli kazi zimeendelea zikifanyika. Baada ya Bunge hili naomba tuwasiliane ili tuweze kuona tunafika pamoja katika miradi hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Mathayo David.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua mradi mkubwa wa maji tambarare ya Mwanga mpaka Same unakamilika lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mathayo, Mbunge wa Same kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni mradi mkubwa, utekelezaji wake unaendelea, pamoja na changamoto zake, Wizara inaendelea kuona tunafanya kila linalowezekana mradi uweze kukamilika na lengo la matumizi haya kwa wananchi wa Same, Mwanga mpaka Korogwe yaweze kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 127

**Barabara ya Kyatema – Kanazi – Ibwela – Katoro – Kyaka**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Kyatema – Kanazi – Ibwela – Katoro – Kyaka kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukizo, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kyatema – Kanazi – Ibwela – Katoro – Kyaka yenye urefu wa kilometa 60.6 umekamilika mwezi Oktoba, 2022. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, inaonesha kwamba Serikali huenda haifahamu vizuri barabara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inahudumia kata 18 za Bukoba, inahudumia wilaya mbili; Wilaya ya Bukoba na Wilaya ya Misenyi, inahudumia nchi mbili; inaziunganisha Tanzania na Uganda na vita ya mwaka 1978 ya Iddi Amini ilipiganwa kwa kutumia barabara hii.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari baada ya Bunge hili kwenda Bukoba kuangalia barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika barabara hiyo kuna Daraja la Kalebe, daraja kubwa ambalo ni la zamani sana, ni bovu, linaruhusiwa uzito wa tani saba, lakini kwa vile hakuna ulinzi wala kizuizi wanapita magari ya tani 15 mpaka 20.

Je, tunasubiri watu wafe pale ndio mtengeneze daraja hilo na barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rwekiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri Mheshimiwa Mbunge amekuja mara kadhaa Wizarani akifatilia ujenzi wa barabara hii pamoja na daraja lake. Kwa niaba ya Serikali napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ya kwamba nipo tayari kuongozana naye kwenda jimboni Bukoba Vijijini ili nikashuhudie na kuona barabara hii pamoja na daraja hili mara baada ya vikao hivi vya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili suala la Daraja la Kalebe ni sehemu ya barabara hii ya kutoka Kyatema-Kanazi, Bwela, Katoro – Kyaka; na kwa maana hiyo kwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekwishakamilika na mwaka ujao wa fedha tumeweka mapendekezo kwamba barabara hii na daraja hili vijengwe.

Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge bajeti yetu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ikifika aipitishe ili pia daraja tuweze kulijenga, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuiuliza Wizara, wananchi wa Mkoa wa Mbeya wanataka kujua ni lini barabara ya njia

nne itaanza kujengwa ambayo ilisaidiwa kwamba kuanzia Uyole mpaka Mbalizi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua umuhimu wa barabara hii ya Mbeya mpaka Tunduma na tayari Serikali ilikwishaitangaza na mkandarasi amepatikana na tunachosubiri na hata kwa maelekezo yako ni kwamba hivi karibuni hususan ndani ya mwezi huu wa pili tutasaini mkataba ili barabara hii ianze kujengwa kwa njia nne kama ambavyo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alivyoahidi alivyotembelea Mkoa wa Mbeya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 128

**Barabara ya Mziha – Kibindu – Mbwewe**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara ya Mziha – Kibindu – Mbwewe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, kunahitajika kufanyika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Mziha – Kibindu – Mbwewe yenye urefu wa kilometa 68.63. Baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na gharama za ujenzi kujulikana Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru pamoja na majibu ya Serikali ambayo pamoja na kwamba hayatoi matumaini ya karibuni, lakini napenda nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali kwamba barabara hii iko chini ya *TANROADS* kwa matengenezo ambayo yanaendelea inawezesha walau kupitika na barabara hii ni *shortcut* kwa ajili ya kutoka Magila – Turiani – Mziha - Handeni - Mziha, Kibindu -Mbwewe kwenda Mikoa ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niulize maswali yangu kama yafuatavyo; je, Serikali ipo tayari kuielekeza *TANROADS* katika matengenezo yanayoendelea kutenga pesa kwa ajili ya matengenezo ya mifereji, kwa sababu eneo hili lina mvua nyingi ili barabara hii iendelee kupitika na kwa kuwa kuna vyakula vingi katika eneo hilo ili uweze kufika sokoni?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa Serikali imepanga mpango mzuri wa kuendelea na upanuzi wa ujenzi wa njia sita kutoka Kibaha mpaka Chalinze na ilishafanya tathmini; je, Serikali inasemaje ina mpango gani

juu ya fidia kwa maeneo ambayo barabara hiyo itapita? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii kwanza ina umuhimu mkubwa sana kwa mikoa hii yote miwili ya Morogoro pamoja na Pwani, na katika mwaka huu wa fedha ili iweze kupitika tumetenga fedha takribani kiasi cha shilingi milioni 346.981 na wakandarasi wawili wapo *site*.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba suala la ujenzi wa mifereji pia tutajenga kwa kuwa tayari wakandarasi wako *site* ni sehemu ya *scope* ya kazi tuliyompatia mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa ajili ya barabara kutoka Kibaha – Chalinze kuja Morogoro kwa ajili ya fidia, tayari barabara hii wizara imekusudia tutafanya kwa mfumo wa *EPC+Finance,* lakini sasa tumebadilisha kwa tutafanya kwa njia ya *Public Private Partnership (PPP)*. Tayari mtaalam mwelekezi Kampuni kutoka Korea ya Kusini yupo *site* na tunategemea tutakabidhi kazi hii kati ya mwezi wa tatu ama wa nne na kupitia ripoti atakayoleta kwa ajili ya fidia na gharama zote, Serikali itatumia hiyo ripoti kwa ajili ya kulipa wale wote watakaokuwa wameathirika na barabara hii, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona mmesimama, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu maswali hayo kwa niaba ya Naibu Waziri wa Ujenzi, kwa hiyo, nafikiri maswali aliyoulizwa yanatosheleza kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni sasa aulize swali lake.

Na. 129

**Kuongeza uzalishaji wa mafuta ya alizeti nchini**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali isiongeze uzalishaji wa mafuta ya alizeti nchini kwa ajili ya Soko la Zanzibar na Bara kuliko kuagiza kutoka nje ya nchi?

(b) Je, hali ya uzalishaji wa mafuta ya alizeti ikoje kwa mwaka na ni mikoa gani inayozalisha zaidi Tanzania Bara?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta nchini kwa lengo la kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula na kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 700,000 hadi tani 1,500,000 ifikapo mwaka 2025. Utekelezaji wa mpango huo unajumuisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya mbegu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo ambapo kwa mwaka

2022/2023 jumla ya shilingi bilioni 43.03 zitatumika kwa lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni tani 650,000 kwa mwaka. Tathmini ya mwaka 2020/2021 inaonesha kuwa uzalishaji wa ndani wa mafuta ya alizeti ni asilimia 75 ya kiasi cha wastani wa tani 300,000 za mafuta ya kula yanayozalishwa nchini kwa mwaka. Mikoa inayozalisha alizeti kwa wingi ni Singida, Dodoma, Manyara, Shinyanga, Iringa, Tabora, Morogoro, Ruvuma, Mbeya, Arusha, Lindi, Mtwara, Rukwa na Mara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ningependa kujua kwa vile kuna taasisi ya *ASA* ambayo Serikali iliipa dhamana ya kutoa mbegu katika msimu wa mwaka 2020/2021; zile mbegu hazikufanya vizuri na wakulima wengi ambao wamezitumia zile mbegu wamepata hasara.

Je, nini kauli Serikali katika kuwafidia wale wakulima ambao wamekula hasara kutokana mbegu zile za taasisi ya *ASA? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali mmejipangaje sasa kuhakikisha haitokei tena wakulima wadogo wadogo ambao wanapata mbegu kutoka taasisi ile ya *ASA* wakaingia tena hasara ili wakaendelea kuwa maskini zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika msimu alioutaja Wakala wa Mbegu za Kilimo *(ASA)* alisambaza mbegu za

alizeti ambazo katika baadhi ya maeneo zilifanya vizuri na pia katika baadhi ya maeneo hazikufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, ziko sababu nyingi zilizopelekea kutokufanya vizuri hasa kutokana na misimu ya kupanda na changamoto zingine zilizosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Iko mikoa ambako mbegu hizi zilistawi vizuri na wananchi wamevuna, wamepata mavuno makubwa na tumekuwa tukichukua kama sehemu ya kielelezo.

Mheshimiwa Spika, katika kuitatua changamoto hii katika mwaka huu wa fedha wa 2022/2023 Serikali imetenga fedha kuhakikisha kwamba tunazalisha mbegu, tunazigawa kwa ruzuku kwa wakulima ambazo ni *certified seed* tofauti na zile ambazo zimewekwa awali na lengo letu ni kuhakikisha kwamba wakulima wazipate mbegu hizi kwa bei rahisi ya ruzuku kwa kilo mbili kwa shilingi 10,000 ili ziweze kuwasaidia kutokana na changamoto ambayo waliipata.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumehakikisha kuanzia hivi sasa tumempa maelekezo *ASA* tutaanza kuzalisha *certified seeds* ili wakulima wetu waweze kulima na waweze kupata tija kutokana na kilimo cha alizeti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, siku za karibuni kupitia vyombo vya habari tumeshuhudia mama mmoja ambaye alifika Zanzibar akiwa na ndizi na alipigwa faini, akatakiwa arudi na bidhaa hiyo upande wa Bara. Lakini wote tunaelewa kwamba Tanzania ni nchi moja.

Ni nini kinasababisha kwamba bidhaa kama hizo zikienda upande wa pili zinarudishwa na nini kauli ya Serikali kwenye hili? Na je, bidhaa...

**SPIKA:** Swali la nyongeza ni moja Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Hata hivyo hii hoja ya huyu mfanyabiashara ndizi zake pengine kurejeshwa ama kukataliwa na kitu kama hicho haiku chini ya Wizara ya Kilimo, nadhani ni hoja ya biashara na ni jambo ambalo linaweza kuzungumzwa katika ya hawa wa biashara na watu wa Wizara yetu inayoshughulikia Muungano chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kwa hiyo, nadhani Serikali itakuwa imelisikia ilifuatilie jambo hilo ili tupate muafaka mzuri.

Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kufahamu ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuimarisha soko la zao la vanila mkoani Kagera? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli zao la vanila hivi sasa limeanza kupata muamko mkubwa na wakulima wengi wamehamasika kulima zao hili na sisi kama Serikali

tumeendelea kufatilia hatua kwa hatua kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira bora na wezeshi kuwafanya wakulima wetu waweze kunufaika na zao hili.

Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni sehemu pia ya mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunatengeneza miundombinu rafiki na mazingira rafiki ili wakulima wetu waweze kunufaika na uzalishaji wa zao la vanila.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburus Saputu, Mbunge wa Arumeru Mangaribi sasa ulize swali lake.

Na. 130

**Mkakati wa kutoa chakula cha bei nafuu kwa wananchi**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-
Je, kuna mpango gani wa kutoa chakula cha bei nafuu kwa wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi kutokana na athari za ukame?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* imeendelea kutoa chakula na kukiuza chini ya bei ya soko. Hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2023 kiasi cha mahindi tani 24,975.152 zimepelekwa na kuuzwa katika Halmashauri 60 nchini katika vituo vya mauzo 116. Halmashauri ya Arumeru, kituo cha mauzo kimefunguliwa

eneo la Kikatiti na jumla ya tani 6.28 zimeshauzwa kwa Wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Saputu swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwanza niombe kusikitika kidogo kwa sababu majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri sio ya jimbo langu. Eneo la Kikatiti liko katika Jimbo la Arumeru Mashariki, kwa hiyo, Waziri amejibu majibu ambayo sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo ningeomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Saputu, kama majibu ya msingi yaliyotolewa unasema sio majibu yenye uhalisia, maswali ya nyongeza hayawezi kusimama juu ya majibu ambayo sio halisia kwa swali uliloliuliza, ndio maana yake.

Kwa hiyo, mimi nitalifatilia hili swali lako litajibiwa tena wakati mwingine nikishajiridhisha kwamba sio majibu sahihi, lakini kama kuna usahihi utapewa fursa ya kuuliza maswali wakati huo. Nadhani tumeshawahi kufanya hivyo humu ndani kwa swali la Mheshimiwa Almas Maige.

Kwa hiyo wewe huwezi kuuliza maswali ya nyongeza juu ya majibu ambayo unasema hayajajibu swali lako. Kwa hiyo inabidi nikajiridhishe haya maswali, swali ulilouliza majibu yaliyotolewa kama ni uhalisia utapewa sasa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza wakati huo na kama haya sio ya uhalisia basi tutataka yaje sasa ya uhalisia halafu ndio upewe nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, nadhani umenielewa.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, swali limejibu hasa kuhusu njaa, lakini eneo ambalo amelizungumzia sio Arumeru Magharibi ndio hasa hoja yangu.

**SPIKA:** Sasa wewe si ni Mbunge wa Arumeru Magharibi na unataka jibu lizungumzie Arumeru Magharibi?

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Kama ndivyo, majibu yamejibu kuhusu eneo ambalo sio la jimbo lako na wewe unataka majibu ya jimbo lako ama ili tuendelee nalo wewe sema wapi panarekebishwa kwenye haya majibu ili ndio nijue jibu liko sahihi lakini kuna neno dogo tu limekosewa.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, amesema amefungua kituo katika eneo la Kikatiti ambalo liko katika Jimbo la Arumeru Mashariki na sio Jimbo la Arumeru Magharibi.

**SPIKA:** Sasa si ndio jibu la msingi hilo. Sasa utauliza maswali yako ya nyongeza kwenye jibu lipi Mheshimiwa? Kwa sababu kama eneo lililo jibu unasema sio la kwako labda ukubali kwamba ni la kwako amekosea kutaja. Kama eneo sio la kwako maana yake sio jibu la swali lako ndio nachojaribu kukusaidia wewe mwenyewe.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, atakuwa amekosea eneo.

**SPIKA:** Eneo sio la kwako?

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Ahsante sana basi swali lako litajibiwa upya. Kwa hiyo, utapata nafasi ya kuuliza maswali yako ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri kuna watu wengine walitaka kuuliza maswali, lakini kwa sababu hayawezi sasa kusimama kwa haya majibu yaliyotolewa.

Mheshimiwa Waziri naona umesimama.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, sisi tunapopeleka chakula tunapeleka kwenye Wilaya, Wilaya inaweza ikawa na majimbo mawili, kituo kinateuliwa na Ofisi ya Kamati ya Ulinzi ya Wilaya. Kwa hiyo kituo kinaweza kikawa kimewekwa kwenye jimbo la 'A' lakini ni sehemu ya Wilaya hiyo moja. Kwa hiyo Kikatiti ni sehemu ya Arumeru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Saputu kwa ufafanuzi huo wa Mheshimiwa Waziri jibu hili linajibu swali lako maana hawa hawaleti kijimbo wanaleta kiwilaya. Kwa ufafanuzi huu jibu hili la msingi linajibu swali lako?

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa mantiki ya Waziri ni kwamba eneo hilo liko Wilaya ya Arumeru.

**SPIKA:** Haya uliza maswali yako mawili ya nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Arumeru hususan Kata 13 ambayo ndio imekubwa na njaa imepakana na Longido, Ngorongoro na Monduli. Katika Wilaya hizo za Ngorongoro, Monduli na Longido chakula kimeuzwa shilingi 700 kwa wananchi, lakini katika upande wa Arumeru Magharibu chakula wananchi wanaambiwa wanauziwa shilingi 885.

Je, ni kwa nini bei katika Wilaya zingine ni shilingi 700 na Arumeru Magharibi ni shilingi 885 na wakati tuko sehemu moja na hali ni hiyo hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa kuna hilo tatizo Waziri haoni haja ya kufika katika Jimbo la Arumeru Magharibi au Wilaya ya Arumeru ili aweze kuona hali halisi ilivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa sijaelewa nani anajibu naona mnarushiana kitenesi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO**: Mheshimiwa Spika, najibu mimi.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza hapa tulishawasiliana naye na tulitoa ufafanuzi ambao nataka niurudie hapa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ya Mheshimiwa Mbunge ni juu ya kituo kuwepo katika eneo ambalo haligusi katika jimbo lake na hivyo wananchi katika eneo lake wanachukua umbali mrefu na bei imekuwa ikiongezeka sana kuweza kupata ile bei ambayo maeneo mengine wanapata.

Mheshimiwa Spika, nilishasema hapa Bungeni ya kwamba katika mazao haya ya mahindi ya bei nafuu, chakula cha bei nafuu kama Mheshimiwa Waziri alivyosema tunapeleke kwenye Halmashauri ya Wilaya na vituo ndiyo vinatengenezwa hapo, lakini ikitokea kwamba katika baadhi ya maeneo kuna umbali mrefu, *NFRA* tumeshawapa maelekezo ya kusogeza vituo hivyo ili kuweza kuwahudumia watu wote kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika maelezo ya awali kama katika eneo lake alikuguswa mimi nitatoa maelekezo siku ya leo kuhakikisha kwamba *NFRA* wanaongeza vituo ili na jimboni kwake pia paweze kuguswa na iweze kupunguza pia hali ya bei kwa sababu moja kati ya changamoto kubwa

inayosababisha pia ni kwa sababu ya umbali ambao wamekuwa wakiupiga *NFRA*.

Kwa hiyo, kwa ujumla wake tumwachie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tutahakikisha pia katika uongezaji wa vituo tutagusa na jimbo lake ili wananchi wake wasiende umbali mrefu na bei pia isiweze kuwa kubwa kama ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ameuliza kuhusu kwenda kujiridhisha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kwenda kujiridhisha hiyo ni kazi yangu mimi kama Naibu Waziri, nilitaka nimhakikishie kwamba nipo tayari baada ya Bunge hili nitakwenda katika eneo hilo kwenda kujiridhisha katika hali ambayo ameisema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa Serikali imetuletea mahindi kwenye vituo viwili kwa maana ya Segese na Isaka na kuacha kata zingine 16 ambazo ziko umbali mrefu kutoka kwenye kata zile.

Sasa swali langu ni lini Serikali itaongeza kiwango cha mahindi na kuwatuma *NFRA* waje waongeza idadi ya vituo kwenye kata?

**SPIKA:** Mheshimiwa unatakiwa uulize swali moja, ni swali la nyongeza. Moja kati ya hayo mawili unataka lipi ujibiwe?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni lini Serikali itawatuma *NFRA* kuja kuongeza idadi ya vituo kwenye kata ambazo ziko mbali na maeneo hayo husika?

**SPIKA:** Haya ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa chakula cha bei nafuu Halmashauri husika huwa wanatuambia eneo ambalo limeteuliwa, lakini kutokana na changamoto za wananchi wetu wanatoka maeneo ya mbali tumeishatoa maelekezo kwa *NFRA* kuhakikisha kwamba wanaongeza vituo zaidi ili wananchi wengi waweze kuhudumiwa kwa ukaribu. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba katika Jimbo la Msalala tutazingatia pia hiyo ili wananchi wake wasitembee umbali mrefu kufuata chakula hiki cha bei nafuu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Halmashauri ya Mji wa Bunda kuna wananchi wanaishi zaidi ya kilometa 40 kuja Kata ya *Bunda Store* ambapo ndipo kituo cha kuuzia mahindi kilipo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kituo kingine cha usambazaji mahindi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chacha Maboto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba kutokana na mahitaji hayo nitatoa maelekezo kwa Wakala wa Hifadhi ya Chakula

kuhakikisha wanaongeza kituo kingine zaidi ili wananchi wasitembee umbali mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa sasa aulize swali lake.

Na. 131

**Kukamilisha Hospitali ya Kanda ya Kusini – Mtwara**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, ni lini Hospitali ya Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara itakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Mollel majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la huduma za mama na mtoto katika Hospitali ya Kanda ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hospitali hii inatoa huduma ya wagonjwa wa nje *(OPD)* na wagonjwa wa kulazwa *(IPD)*. Aidha, Serikali itaendelea kuipa hospitali hii kipaumbele katika mpango wa bajeti ili kuhakikisha kuwa inakamilika ifikapo mwaka 2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya swali la nyongeza.

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwanza nishukuru na niipongeze Serikali kwa jitihada inayofanyika kwa ajili ya kuendeleza hospitali hii.

Mheshimiwa Spika, hospitali hii ni tegemeo kubwa sana kwa watu wa Kanda ya Kusini ambao wanalazimika kutembea umbali wa kilometa 1,200 kwa mfano kutokea Mbamba Bay mpaka Dar es Salaam kufuata hizi huduma kutokana na pale kutokuwa na huduma kamilifu. Hospitali hii haina *ambulance,* haina gari ya Mkurugenzi, haina chumba cha kuhifadhia maiti, hospitali hii *OC* yake ni ndogo sana lakini ndiyo Hospitali ya Kanda.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka jicho la kipekee katika hospitali hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; sambamba na hilo watumishi pia wako wachache, lakini tayari kumeshakuwa na msongamano na pia kupunguza msongamano ambao pia unaelekea katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya.

Je, ni lini Serikali itaongeza idadi wa watumishi ili kuondoa hadha hii ambayo imeendelea huko? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mbunge kwa namna ambavyo anafatilia masuala ya huduma kwenye kanda yake, lakini pia tumepokea barua yake kuhusu vifaa vinavyohitajika na Wilaya yake, pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakinio niseme kwamba moja kwanza ieleweke kwamba hospitali hii ya kanda ni hospitali ambayo sasa ndiyo inaenda kufikisha miaka miwili toka izinduliwe na

Makamu wa Rais na kwa kibali cha mwaka huu tumepeleka kuomba kuajiri watumishi 111; lakini kwa sasa wako watumishi 166.

Mheshimiwa Spika, lakini pia amezungumzia suala la *ambulance;* kwa hospitali hii ya kwenu katika *ambulance* 727 ambazo Rais wetu ametoa fedha kwa ajili ya kununua *ambulance* iko kwa ajili ya hospitali hii ya kwenu.

Mheshimiwa Spika, lakini amezungumzia suala la *mortuary* na mengine; shilingi bilioni 4.4 ambazo ninazungumzia hapa tayari manunuzi yameanza kufanyika kwa ajili ya ujenzi wa *mortuary*, ujenzi wa nyumba za wanyafakazi, umaliziaji wa maabara lakini umaliziaji wa jengo la mama na mtoto.

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hospitali hii itaenda kuwa ni nzuri na unajua we mwenyewe kwamba katika hospitali zote za kanda nchini hospitali hiyo ndiyo ina majengo mazuri kuliko hospitali yoyote, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri..., aah, Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; kwa kuwa Singida Mjini hatuna Hospitali ya Wilaya na kwakuwa Wizara ya Afya ilikuwa tayari kutukabidhi Hospitali ya Mkoa kwa maana ya yale majengo ya Mkoa ili tuanzishe Hospitali ya Wilaya. Sasa nataka kujua ni lini mtatukabidhi hayo majengo ya Mkoa tuweze kuanzisha Hospitali ya Wilaya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anaposema Mheshimiwa Mbunge Hospitali ya Mkoa iko sasa

hivi kwenye eneo ambalo Hospitali ya Wilaya ndiyo inatakiwa iwepo na sasa kuna majengo mengine ambayo yanaendelea kujengwa kwenye eneo lingine. Lakini Mheshimiwa Mbunge ni kweli tuna majengo yanamaliziwa siyo muda mrefu ili Hospitali ya Mkoa iweze kuhama lakini nikuhakikishie tuna shida hiyo kule Geita, pale kwako tutahama polepole kwa sababu ukiama ghafla haraka haraka unaweza ukavuruga shughuli za tiba kwenye eneo lako, ili tusikuharibie siasa yako kabla ya mwaka 2025 tunamalizia majengo, tutahama polepole, lakini tutahakikisha kwamba hatutavuruga shughuli zako, cha msingi wape ushirikiano lile lile eneo na mshirikiane kwa pamoja kuweza kutoa huduma.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba. Mheshimiwa Naibu Waziri geukia upande huu. Mheshimiwa Shamsia Mtamba swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza tunaishukuru sana Serikali kwa hatua iliyofikia katika hospitali yetu ya Kanda ya Kusini, lakini tumekuwa na changamoto kubwa sana ya Madaktari Bingwa. Je, ni lini sasa Serikali itatuletea Madaktari Bingwa katika hospitali yetu hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hospitali ile inahitaji Madaktari Bingwa. Kuna Madaktari Bingwa, lakini Madaktari Bingwa kwa kiwango kinachohitajika kwa Hospitali ya Kanda bado hawajafikia hicho kiwango. Sasa upembuzi yakinifu unafanyika kuweza kuainisha maeneo mengine ili kuamisha na kupeleka kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika hivyo hata hivyo cha kwanza tulikuwa tunangojea kukamilisha baadhi ya miundombinu hapa karibuni ndiyo *CT-scan* imekwenda na *MRI* mashine, sasa hata ukiwahamisha wataalam wa kibingwa wanaweza wakapata vifaa vya kufanyia kazi ndiyo maana hawajaweza kupelekwa mapema katika eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, mliosimama mketi, ninayo matangazo hapa mbele tutaanza na tangazo la wageni.

Waheshimiwa Wabunge, mnaoingia mnapaswa kusubiri mpaka nimalize kuzungumza.

Wageni walioko Jukwaa la Spika kwanza ni wageni wangu yupo; Naibu Rais wa Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) Dkt. Mussa Mohamed Hans, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huyu ni Naibu Rais na humu ndani tunae mwenyewe Mheshimiwa Salma Kikwete, ndiyo bosi wake, yeye ndiye Rais wa Chama hiki duniani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mgeni huyu amekuja na Tuzo ya Uenezi wa Kiswahili kwa ajili ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala ya Bunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo Bunge letu leo litapokea tuzo hiyo ya kueneza Kiswahili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile pia ameongozana na Katibu Mtendaji wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) Consolata Mushi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni Ndugu Rahel Gwivaha na Ndugu Sabrina Said, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni wenu ambao wametufikia leo hapa; tunao wageni watano wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama cha Mapinduzi na Umoja wa Vijana Chama cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Uzini, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni Wajumbe wa Shirikisho la Vikundi vya Ujasiriamali Tanzania (SHIVUTA) kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 24 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate ambao ni Kwaya ya Kitimtim kutoka Kanisa ya Anglikana, Area E - Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 50 wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ambao ni walimu watano na

wanafunzi 50 kutoka Shule ya Msingi ya *St. Therese of Lisieux* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambao ni wawekezaji kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 12 wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambao ni wapiga kura wake na viongozi kutoka Msalala, Mkoa wa Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Clephes Lufungo. Nadhani huyu ameandikwa mara mbili; Ndugu Clephes Lufungo, mgeni wa Mheshimiwa Shangazi, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambao ni wapiga kura wake kutoka Babati, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Khadija Taya ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Condester Sichalwe ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Antonia Nsimbi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunaye Naibu

Meya Mstaafu wa Ilala Mheshimiwa Mohamed Yakubu na Ndugu Naftali Koba, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wawakilishi 22 wa Chama cha Skauti Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi saba kutoka Shule Kuu ya Sheria Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi watano kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Mkongo Maulid, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 70 na walimu watano kutoka Shule ya Msingi *Assumption* ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 30 na walimu sita kutoka Shule ya Sekondari Charlotte ya Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Wajumbe 35 wa Baraza la Jumuiya ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi Kata ya Kamara na Saranga kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe cha Mkoani Morogoro. Huyu ni mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe cha Mkoani Morogoro Ndugu Frank Alexander, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo la wageni; ninayo mambo machache kwanza ni jambo ambalo liliombwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango siku ya tarehe 7 Februari, 2023.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 7 Februari, 2023 katika Kikao cha Sita cha Mkutano wa Kumi wa Bunge alisimama Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri wa Fedha na Mipango kuomba kuhusu utaratibu chini ya Kanuni ya 75 na 71 za Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba aliomba kuhusu utaratibu wakati Mheshimiwa Katani Katani akitoa mchango wake katika Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya *(PIC),* Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kwa mwaka 2022.

Waheshimiwa Wabunge, katika mchango wake kama ulivyorekodiwa katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* Mheshimiwa Katani alisema nanukuu; "Mimi nawaambia fanyeni tathimini ya kina tunakwenda wapi? Kuna mambo unapaswa umwambie mtu mdogo sana, Mwigulu kaka yangu na rafiki yangu umetutukana Wabunge sana, mimi nakuambia umetutukana Wabunge sana na unapaswa ukae na utafakari utakapokaa, hapa hakuna anayeweza kujadili waganga wa kienyeji hapa hamna, hamna.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya tunayojadili ni maisha ya Watanzania na tumeletwa Bungeni tuwasaidie Watanzania."

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na kauli hiyo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu alisimama na kuomba Kuhusu Utaratibu chini ya Kanuni ya 75 na 71 za Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, alieleza kuwa Mbunge aliyekuwa anachangia alisema uongo nanukuu; "Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maslahi ya muda ninaomba Mbunge anapochangia kanuni yetu inazuia kusema jambo la uongo, sasa Mheshimiwa Mbunge anapo-*generalize* kwamba mimi nimewatukana Wabunge hiyo ni *allegation* kubwa sana ambayo Bunge lako

haliruhusu na mimi nisingeweza kutukana Wabunge na Kiti kikiwepo."

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 75(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kiti kilitoa maelekezo kuwa uamuzi Kuhusu Utaratibu ulioombwa utatolewa baadaye.

Baada ya kuzipitia Taarifa Rasmi za Bunge nimetambua kwamba chimbuko la kauli ya Mheshimiwa Katani A. Katani na kauli za baadhi ya Wabunge wengine ambao wamekuwa wakizitoa hapa Bungeni kuhusu jambo hili zinatokana na kauli ya Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa Fedha na Mipango aliyoitoa mnamo tarehe 1 Februari, 2023 katika Kikao cha Pili cha Mkutano wa Kumi wakati akichangia Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Taarifa ya Kamai ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022. *(Makofi)*

Katika mchango wake Mheshimiwa Waziri alitolea ufafanuzi hoja ya Mheshimiwa Luhaga Mpina alizokuwa ameziibua wakati akichangia Taarifa za Kamati hizi.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alisema kama ifuatavyo na nanukuu; "Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niweke kumbukumbu sawa katika baadhi ya mambo ili *Hansard* zako ziweze kupata vizuri. Nikianza na jambo moja ambalo ameliongelea Mheshimiwa Mpina, katika mchango wake amechangia mengi, lakini eneo mojawapo amesema, tunapata mfumuko wa bei kwa sababu ya *mis-management* ya sera za fedha, akaelezea kwamba tumefanya malipo nje ya bajeti. Kwa maana hiyo, yeye akakichukulia hicho kama kitu ambacho ni *mis-management* ya sera za fedha."

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri alitolea ufafanuzi hoja hii na hoja nyingine za mchango wa

Mheshimiwa Mpina kwa kirefu na wakati akimaliza alisema na nanukuu; "Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujadili mambo mengine huko yanayohusu uganga wa kienyeji na vitu vingine, kwenye uchumi *this is my profession,* tunajadilije hivi vitu ambavyo vipo *clear?" (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kauli hii ndio iliyozua mtafaruku miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge na kuona kuwa wametukanwa. Ndio maana katika mchango wa Mheshimiwa Katani ambao nimeshaunukuu hapo juu akawa ametumia hayo maneno kwamba umetutukana Wabunge sana, lakini pia baadhi ya Wabunge katika michango yao wameonesha kuguswa na kauli hii kwa mtazamo hasi, hivyo wamekuwa wakiirejea katika michango yao hapa Bungeni kama ishara ya kutoridhishwa na kauli hiyo.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliomba Kuhusu Utaratibu akisema kwamba jambo hilo ni la uongo. *(Makofi)*

Sasa baada ya kuzipitia Taarifa Rasmi za Bunge kama nilivyonukuu hapo juu, ni dhahiri kwamba maneno hayo Mheshimiwa Mwigulu aliyasema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kanuni zetu hasa masharti yaliyowekwa chini ya Kanuni ya 71 yanataka Bungeni tutumie lugha ya staha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwigulu ni dhahiri ukiisoma kwa sababu hapa nimechukua kwa kifupi, ukisoma ule mchango wake na sisi Wabunge huwa tunafanya hivyo na ninasema hapa kwa kirefu ili tuelewane vizuri.

Sisi Wabunge pia, wakati mwingine tukiwa tunachangia, hatuchangii hoja tunaenda kushughulika na mtu binafsi, kwa hiyo na yeye Waziri ama Naibu Waziri anaposimama kujibu hoja analazimika kwenda kwa mtu mmoja badala ya hoja alizozisema. Kwa hiyo, pande zote mbili kwa mwongozo huu

nitakaotoa leo, kila upande ufanye yale unayopaswa kulingana na kanuni zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuchangie hoja badala ya kuchangia kuhusu mtu, lakini pia Waheshimiwa Mawaziri wajibu hoja badala ya kujibu mtu kwa sababu lengo ni dhahiri la Mheshimiwa Mwigulu alikuwa akimjibu Mheshimiwa Mpina, lakini kwa sababu alieleza maelezo marefu hapo katikati baadae ndio akaja kusema hii sentensi ikaonekana kana kwamba inalihusu Bunge zima, na ndio maana Wabunge wamekuwa wakisimama wakiirejea ile kauli. Lakini kimsingi yeye alikusudia kumjibu mtu mmoja ambaye na yeye alikuwa amezungumzanaye kwa namna alivyoona yeye kwamba haistahili. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu Kanuni yetu ya 71 inataka tutumie hiyo lugha ya staha, lakini pia kwa ajili ya kulinda haki ya Waheshimiwa Wabunge ambayo imetolewa chini ya Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kwamba wanao uhuru wa mawazo na majadiliano ili waweze kuihoji Serikali na kuisimamia, hivyo uamuzi sasa wa Kiti kwa sababu haukuwa umeombwa Mwongozo ulikuwa umeombwa Utaratibu, kujua kama kanuni imekiukwa au hapana, lakini kwa sababu pia maneno haya yameendelea kujadiliwa hapa Bungeni na hili sasa lifike mwisho, hayo maneno aliyokuwa ameyasema Mheshimiwa Mwigulu kwamba; "hebu tujadili mambo mengine huko yanayohusu uganga wa kienyeji na vitu vingine, kwenye uchumi *this is my profession,*" yafutwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Na huo ndio uamuzi wa Kiti kuhusu Utaratibu uliokuwa umeombwa na Mheshimiwa Mwigulu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo niko nalo hapa mbele, kama mnavyofahamu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa mwaka 2022 ulipangwa

kuingia Bungeni kwa maana ya Bunge hili kwa hatua zake zote katika Mkutano wetu huu wa Kumi. Hata hivyo bdo majadiliano katika ngazi ya Kamati yanaendelea kwa lengo la kuuboresha zaidi, hasa katika eneo la mambo yanayohusu bajeti, ama mambo ya kifedha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hivyo Muswada huu wa Bima ya Afya kwa Wote wa mwaka 2022 utawasilishwa wakati mwingine Kamati itakapokuwa imeshakamilisha kujadiliana na Serikali kwenye mambo ya kifedha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo hapa mbele, mnatangaziwa na Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwamba Wabunge wote wa CCM kutakuwa na kikao cha Wabunge hao leo siku ya Alhamisi mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge hapa ama kuahirisha shughuli za Bunge. Kwa hiyo, asubuhi hii Wabunge wa CCM wataelekea Ukumbi wa Msekwa.

Lakini Waheshimiwa Wabunge, hapa aliuliza swali Mheshimiwa Paresso kuhusu ndizi kule Zanzibar na nikasema kwamba Waziri aliyekuwa amesimama hapa kwa sababu alikuwa ni Naibu Waziri wa Kilimo, swali hilo lilikuwa halimhusu yeye.

Sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira yuko tayari na majibu ya swali hilo lililoulizwa na Mheshimiwa Paresso, hivyo nitampa fursa ya kujibu swali hilo.

Mheshimiwa Waziri au unaweza kujibia hapo mbele kwa sababu unajibu swali, usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nishukuru kwa busara yako njema ya kuongoza Bunge letu hili tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la dada yangu Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dada Paresso alizungumza suala zima la kuzuiliwa kwa ndizi za mama mmoja wiki iliyopita ambapo Watanzania walishuhudia jambo lile likitokea katika mitandao ya kijamii. Na kweli mimi mara baada ya kuona jambo lile kwa sababu ninahusika na dhamana ya Muungano wetu, lakini nikifahamu kwamba Muungano wetu katika mambo tunafanya vizuri katika upande wa Muungano maeneo yote mawili. Ililazimu ofisi yangu kwa haraka sana kuwasiliana na ofisi ya mwenzangu, Mheshimiwa Hamza, Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili Zanzibar, kumuuliza kulikoni ninachokiona katika mitandao?

Mheshimiwa Spika, Waziri mwenzangu alinijibu ya kwamba jambo hilo ni kweli limetokea, lakini ni kwa sababu kufuatia Tangazo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambalo limetolewa kwa mujibu wa Sheria Namba 9 ya mwaka 1997, Sheria ya Uhifadhi wa Mimea, na tangazo hilo limetokana na hivi karibuni imebainika kuna ugonjwa wa mnyauko wa migomba ambao unaitwa *Banana Xanthomonas Campestris.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kutoa tangazo maalum la kuzuia mazao yote ya migomba ikiwemo ndizi, mimea na majani kwa lengo la kuepusha ugonjwa huo usisambae katika maeneo mbalimbali, lakini wakatoa maelekezo katika maeneo yote ya kuingilia vyombo mbalimbali kuzuia mimea hiyo isiweze kuingia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mujibu wa Sheria hiyo Namba 9 ya mwaka 1997; endapo kosa hilo litabainika kuna adhabu zake tatu, jambo la kwanza aliyehusika kuingiza mimea hiyo anapaswa kuiteketeza kwa gharama zake mwenyewe; ahabu ya pili ni kwamba anaweza akapewa *fine* ya 50,000 kulipa ama zaidi ya hapo na adhabu ya tatu, anaweza akaelekezwa ya kwamba adhabu yake ni kifungo cha miezi sita kwenda gerezani miezi sita ama adhabu zile mbili kwa pamoja. Hii ni kwa mujibu wa Sheria Namba 9 ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tangazo hili lilikuwa limetoka na kuwekwa katika maeneo yote ya kuingilia kwa mipaka ile. Tunafahamu kwamba kila nchi duniani ina utaratibu au kila maeneo mamlaka zina taratibu zake za kulinda.

Kwa hiyo, hili lilikuwa ni suala zima la udhibiti, lakini kwa bahati mbaya mama yule alikuwa hafahamu kwamba kuna lile tangazo lilitoka kabla. Kwa hiyo, ndio maana tulipofuatilia tulipata majibu hayo kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na ni kweli tangazo lile lilitoka kwa kuziia suala zima la ugonjwa wa mnyauko wa migomba usiingie katika upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sisi katika hilo tukaona basi ni vyema tangazo lile likatolewa kwa uwazi zaidi. Lengo kubwa ni kwamba watu wasiofahamu kwamba kuna zuio la kuingiza mazao ya migomba basi kila Mtanzania aweze kulipata kwa ajili ya kuchukua tahadhari hizo.

Mheshimiwa Spika, na hicho ndicho kilichojiri kule Zanzibar. Kwa hiyo, mpaka hivi sasa tangazo lile ni tangazo halali la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, limewekwa kwa ajili ya kuzuwia mimea hasa mazao ya migomba, ndizi zake, migomba na majani yasiingie kwa ajili ya kuzuia suala zima la uambukizaji wa ugonjwa wa mimea hii ya ndizi.

Mheshimiwa Spika, huu ndio mustakabali wa jambo hili. Kwa hiyo, hili wenzetu wameli-*treat* hivyo, lakini ni kwa mujibu wa Sheria ya *Quarantine* kule utaratibu wa kuhifadhi mimea katika eneo hilo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge lako tukufu Wabunge wanatambulika kwa taaluma mbalimbali, wapo ambao ni ma-*engineer* ambao kabla ya jina lake kutajwa linatangulia jina hilo la taaluma yake, lakini pia wapo madaktari ambao ni matabibu na wapo madaktari ambao ni wa kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Kumi na Moja nakumbuka yupo Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum alitunukiwa shahada ya udaktari wa heshima na alileta cheti na Mheshimiwa Spika alimtangaza ndani ya Bunge lako tukufu kwamba sasa atatambulika kama daktari.

Sasa hivi karibuni wapo baadhi ya wenzetu Wabunge wamepata heshima hiyo, lakini bado *status*/hadhi zao zinasomeka vilevile, hawajaweka hiki kianzio kwa maana ya ile taaluma ambayo wameipata.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mwongozo wako, kwanza nataka tufahamu kwamba hivi vyuo ambavyo vinatoa huu udaktari wa heshima ni kwa kiasi gani vinatambulika katika mamlaka zetu zinazosimamia eneo zima la elimu katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeona kwamba baadhi ya Wabunge wana muda mfupi sana, lakini wameweza kutunukiwa hizo *degree* za heshima, lakini wapo Wabunge ambao wana miaka mingi na bado hawajabahatika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sijui ni vigezo gani vinatumika, lakini kwa ujumla wake tungependa kutambua ni kwa kiasi gani mamlaka ambazo zinasimamia elimu zinatambua uwepo wa *doctorate* hizi ambazo zinatolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, mwongozo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wa mwisho huo, Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nilikuwa naomba mwongozo kwa Kanuni ya 76.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mara watu 66 wana kilio kikubwa cha watoto wao kufutiwa matokeo kwa Shule ya Sekondari ya Tuiboki. Watoto 66 wamefutiwa matokeo, walikuwa 67 lakini mmoja ameruhusiwa amepata matokeo yake.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mwongozo, ninachokiona hapa ni kwamba watunga mitihani ni Baraza la Mitihani, watoa mitihani ni Baraza la Mitihani, wasimamizi wa

mitihani ni Baraza la Mitihani, wanaoenda kuangalia watoto wamefanya vizuri siku ya mitihani ni wao wanaweka saini.

Kwa taarifa zilizoko pale ni kwamba walisimamia mitihani ya Shule ya Sekondari Tuiboke na wakaandika pale mitihani imeenda vizuri, sasa watoto wote wamefutiwa mitihani wakiwa na lengo kwamba eti watoto hawa waliangaliana, sijui walikuwa na majibu yanayofanana.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tunataka kujiuliza ni nani anawajibika kwenye suala hili? Kama Baraza la Mitihani ndio watunga mitihani, ndio wanaotunga na ndio wanaosimamia, kama mitihani iliibiwa halafu wanawaadhibu watoto kwa maana ya wazazi wamelipa milioni 12 kwenye shule ya *private,* wao wameadhibika wapi? Na lini sasa watoto hao watafanya mitihani?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama hapa Mheshimiwa Shangazi kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 76 akitaka Mwongozo wa Spika na miongozo yote miwili; na Mheshimiwa Getere hapa kasimama naye ameomba Mwongozo wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 76 inaweka masharti ya jambo gani linaweza kuombewa mwongozo na jambo hilo linapaswa kuwa kwanza linahusu jambo lililotokea humu ndani na unapouliza Mwongozo unataka kujua ikiwa jambo hilo linaruhusiwa ama haliruhusiwi.

Kwa hiyo, ni dhahiri mambo yote mawili yaliyoombewa mwongozo hayajatokea hapa Bungeni, lakini hata hivyo kwa sababu ni mambo ambayo yanaigusa jamii yetu na Mheshimiwa Shangazi anaweza kusema pengine yanatokea humu ndani kila siku kwa maana ya kwamba watu wanatunukiwa huo udaktari wa heshima. *(Makofi)*

Sasa kabla sijatoa maelezo ya ziada kwa sababu nimesema kwanza haiku kwenye hoja ya mwongozo, kwa maana ya matumizi ya Kanuni ya 76, yote mawili kwa sababu, leo hakuna aliyetunukiwa humu ndani halafu akawa na hoja hiyo. Ila Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia yuko hapa, nadhani nimpe fursa atoe ufafanuzi wa mambo hayo yote mawili, halafu mimi nitamalizia sasa maelezo ya jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, naamini uliwasikia ama unataka? Uliwasikia, ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii ya kutoa ufafanuzi kwa mambo mawili ambayo yamezungumziwa hapa.

La kwanza linahusu wanaopata…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ningependa sana tusikilizane kwenye hoja hii. Ni muhimu sana kusikilizana kwa sababu tutafika mahali humu ndani kila mtu atakuwa daktari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni muhimu sana kusikiliza ili ujue kama na wewe ukachukue huko wanakochukua ama usiende, sikiliza maelezo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza kuhusu wanaopewa *PhD*.

Mheshimiwa Spika, kuna namna tatu za kupata *PhD,* kupata hizi *doctorate;* ya kwanza ni ile ya kusomea darasani na kuandika *dissertation.* Unaipata kwa *course work* na *dissertation* na unaipata kwenye chuo ambacho

kinatambulika na vyuo vinatambulika popote duniani na uwezo wetu wa kuvifuatilia vyuo upo popote ambapo utatunukiwa *PhD* kama hiyo au *doctorate* tunaweza tukaifuatilia.

Mheshimiwa Spika, ya pili unaweza ukaipata kwa kufanya *research*, unajisajili kwenye chou, unafanya utafiti unasimamiwa, unaweza usiwe unaenda darasani lakini mara kwa mara unawasiliana na msimamizi wako mpaka unakuja kutunukiwa na kile chuo *PhD* ambayo utakuwa umeipataa kwa sababu ya utafiti uliofanya na chapisho ambalo umelitoa na hilo linaweza likapatikana. Na hapo hapa ukipata hiyo tuna uwezo wa kufuatilia, tunaweza tukahakiki chuo hicho kwa sababu vyuo vyote duniani popote vilipo vinasajiliwa na mamlaka husika katika nchi ambayo inahusika.

Mheshimiwa Spika, namna ya tatu ni hizi za heshima ambazo zinatolewa na ni *tradition* dunia nzima kwamba kuna watu kwa *achievement* zao, kwa michango yao ya aina mbalimbali, chuo kinachotambulika kinaweza kikampa heshima ya kutoa *doctorate* kwa yule ambaye chuo kimemchagua kwa utaratibu unao husika. Kwa mfano nafahamu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tuna utaratibu wake ili mtu aweze kutunukiwa *doctorate* lazima kutolewe *proposal* ndani ya chuo na mtu ambaye anatambulika, lifanyiwe utafiti, lihakikiwe halafu baadae wawasiliane kwa yule ambaye anatakiwa kupata *doctorate* hiyo aende akapate.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa namna zote hizo tatu ukipata kwa mfano kwa kufanya darasani *course work* na *dissertation* au ukapata *by thesis* kwa kuandika *research* au ukatunukiwa, ukiwa unataka kuhakiki au ukitakiwa kuhakiki kile ulichokipata kama ni sahihi, kwa mfano unataka kuomba kazi na mahitaji ya kazi hiyo ni kwamba uwe na *PhD,* mamlaka ambayo inataka kukuajiri inaweza ikataka Serikali

kupitia *TCU* ihakiki *degree* yako kama ni ya kweli na kazi hiyo tunaifanya vizuri sana. Kama umeipata mahali popote sisi tutawasiliana na mamlaka ya nchi ile ambayo umeipata watatuhakikishia kwamba kile ni chuo kikuu kweli, kimesajiliwa, kiko *competent* na kimekuwa *award* na sisi tukishapata hivyo tunampelekea yule anayetaka kukuajiri na kumweleza kwamba kwa hakika hiki chuo kinafahamika. Kama sio chuo kikuu kinachotambulika, kama ni taasisi tu ambayo haijasajiliwa mahali popote lakini imeamua kutoa ile na wewe unataka kuajiriwa kwa ajili hiyo, tukiuliza na tukaambiwa ni taasisi tu lakini haitambuliki kama chuo kikuu tutapeleka kwa mamlaka inayotaka kukuajiri kueleza kwamba huyo katunukiwa na taassi ambayo kwa kweli hatuitambui.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, watu ambao wanatunukiwa, mahitaji yatakapotokea Serikali kupitia *TCU* ifanye uhakiki na tuko tayari kufanya uhakiki na kutambua kwamba nani ameipata, lakini asipokuja sisi huwa hatuingilii, kwamba mtu ametunukiwa na hakuna mahitaji kwetu sisi kwenda kuhakiki kwamba alichopewa kinatokana na taasisi kwamba kweli imesajiliwa kama chuo kikuu sisi hatu-*respond* mpaka tuulizwe. Hilo ni kwa upande wa jibu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi mahitaji yakija kwamba huyu mtu tunahitaji kuhakiki kile alichokipata kama ni *PhD* na amepata na chuo ambacho kinatambulika duniani, kazi hiyo tuna uwezo wa kuifanya vizuri sana. Lakini tukimsikia mtu yuko mahali tu labda amesema ameipata na hatujaulizwa sisi hatuwezi kwenda ku-*verify* kwa kila mtu mahali popote alipo kwa sababu labda amesema amepata *PhD* mpaka tuulizwe na tukiulizwa tutafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mwongozo wa pili kuhusu matokeo ya mtihani.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa ujumla wake kwamba ni vizuri wote tuwe makini sana na suala la mitihani na hasa udanganyifu katika mitihani kwa ujumla wake. Tunapozungumza kuhusu ubora wa elimu ni pamoja na kuhakikisha kwa wale ambao wanafanya *transition* kwa kuchujwa kwa kupitia mitihani, ile mitihani inafanyika kwa ukweli na wanapimwa kwa ukweli bila udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, madhara ya udanganyifu kwenye mtihani ni makubwa sana kwenye mfumo wetu wa elimu, kwenye uchumi wetu na katika maisha yetu. Ukaja ukakuta daktari ambaye kapita kwa magumashi, kwa kudanganya halafu akakutibu wewe au mwanao madhara yake yatakuwa makubwa sana. Kwa hiyo tuna umakini sana wa kufuatilia usimamizi wa mitihani.

Mheshimiwa Spika, kwa hili suala la shule hii ya Mara aliyouliza Mheshimiwa Getere, kilichotokea ni kwamba kuna sababu za kutosha kwamba kulikuwa na udanganyifu katika mtihani. Majibu yana mfanano ambao *statistically* haiwezekani yakafanana bila kuwa na *coordinated effort* ya kuhakikisha kwamba hawa wanajibu kama walivyoelekezwa. Tumeangalia na sisi wenyewe kama Wizara tumekuja kuangalia na kuhakiki kilichokuwa kinatokea.

Sasa swali la msingi alilouliza Mheshimiwa Getere ni kwamba kama imekuwa hivyo, lakini si kuna watu walikuwa wanasimamia mtihani ule. Ilikuaje sasa hawa waonekane kama kweli wana majibu ambayo yanafanana kwa namna ambayo haiwezekani bila *coordination?* Ni hatua gani inachukuliwa? Na la pili mbona mmoja matokeo yake yametangazwa halafu wengine wote ambao walikuwa kwenye lile darasa matokeo yao hayakutangazwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa upande wa hatua ambazo zinachukuliwa, taarifa ambazo nilizipata jana ni kwamba wapo watu 12 wako mahabusu sasa hivi kwa

sababu ya kuvujisha mtihani na hao wako mahabusu *in connection* na shule hii ambayo iko katika Mkoa wa Mara na uchunguzi unaendelea kujua nini kilitokea mpaka hawa wanafunzi wakaweza kuwa na majibu yanayofanana kiasi hicho. *(Makofi)*

Lakini pili, barua zimeandikwa kwa mamlaka ya waajiri wa wale waliosimamia mtihani pale ili wachukuliwe hatua kwa sababu kama kweli tunaona wanafunzi na nitatoa mfano wa shule moja ambao *actually* walivujisha mtihani, walifungua mtihani kabla ya muda, wakawekwa kwenye bwalo la chakula, wakafundishwa ule mtihani, halafu wakaingia kwenye mtihani kwenda kuufanya na hiyo matokeo yake yamefutwa na tunafikiria ile shule kuifutilia mbali, kwa sababu hatuwezi kuruhusu udanganyifu wa namna hiyo.

Kwa hiyo, uchunguzi unaendelea kwa shule hii kujua kwamba wale ambao wamekamatwa tumefikia wapi na wale ambao walihusika kusimamia mtihani ni hatua gani zimechukuliwa ili kuahakikisha tunakomesha mambo haya.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa yule ambaye matokeo yake yametoka, kwa sababu kilichosababisha matokeo yale yafutwe ni ile *pattern* ya majibu ambayo *clearly* yalikuwa ni watu ambao wamekuwa *coached* namna ya kujibu yale maswali na wamejibu *identically* wote kwa pamoja. Yuko mwanafunzi mmoja ambaye kabisa haku-*fit* hiyo *pattern* kabisa, kabisa.

Sasa je, alioneshwa mtihani lakini akaamua kujibu anavyotaka? Hatujui. Je hakwenda kuoneshwa lakini akaingia akajibu? Hatujui.

Kwa hiyo, Baraza la Mtihani likaona kwamba halina sababu za msingi za kuzuia matokeo ya mwanafunzi huyu mmoja tu katika wanafunzi 67, mmoja matokeo yake

yametoka na hawa 66 hayakutoka kwa sababu hiyo ya *base* ya kufanana kwa mtihani.

Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote tusimame kidete kwenye suala hili. Tuhakikishe kwamba wote kwa kweli *professionalism* ya nchi yetu ni muhimu sana tukasimamia taasisi kama Baraza la Mitihani kuhakikisha kwamba linafanya kazi vizuri kwa weledi na tuliache lifanye kazi kwa kutenda haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nimesema na ninarudia tena kusema mbele ya Bunge lako tukufu kwa wazazi ambao wanahisi kwamba kuna uonevu tuko tayari kukutana na wazazi hao mahali popote tuwaoneshe kilichotokea kwa Watoto wao waliokuwa wanasoma pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ameshaeleza Mheshimiwa Waziri kwa kirefu, na mimi nikubaliane naye hasa kwenye hoja hii ya pili. Udanganyifu hauna namna ya kuutetea na sisi kama viongozi ni lazima tuwe na lengo kwamba nchi yetu ikue kielimu, kitaaluma na kila kitu. Kwa hiyo hakuna namna ya kuutetea udanganyifu. Tunachoweza kusisitiza kwa Serikali ni kufanya uchunguzi na kuchukua hatua katika mnyororo mzima wa wale wanaohusika kwenye udanganyifu. Lakini udanganyifu haupaswi kabisa kuvumilika kwa sababu mwisho wa haya hawa ndio wanaokuja kuchukua nafasi hizi zote tulizonazo. Kwa hiyo, ni lazima watu ambao wana huo uadilifu na hawajifunzi udanganyifu kwenye ngazi ile na tunasema wachukuliwe hatua kwa sababu mwanafunzi hana namna ya kuupata mtihani isipokuwa kama amewezeshwa kupata huo mtihani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hao wote waliohusika lakini na yeye pamoja na kwamba anapata hizo athari, lakini sasa anayo nafasi

nyingine ya kufatilia masomo sehemu nyingine ama kwenye shule hiyo hiyo, lakini lazima afanye ule mtihani na ndio maana upo, mpaka itakapofika tutakapoondoa utaratibu wa kupimana kwa mitihani kama Taifa hilo ni suala lingine. Lakini maadam mitihani imewekwa kwa ajili ya kupimana tuendelee kupimana hivyo na tusiutetee kwa namna yoyote ile udanganyifu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwenye hili la kwanza Mheshimiwa Waziri pia ameeleza kwa kirefu hili jambo ambalo limeelezwa na Mheshimiwa Shangazi.

Nafikiri kama Taifa lazima tufike mahali tujue nini tunataka, kwa sababu Mheshimiwa Waziri umesema ninyi hamfatilii yeyote anakopata, lakini kama Taifa athari zake tunaweza tusizione sasa tutaziona baadae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hizi heshima zinazotolewa wala sitaki kurejea kwenye huo mjadala ulishaelezwa kwa kirefu sana na Mheshimiwa Kabudi na ndio hasa lengo la kutolewa zile degree za heshima. Anapopewa Udaktari wa Heshima Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, wamefanya utafiti kuhusu kazi alizozifanya sio tu alipokuwa Rais; wamefanya utafiti wa kazi alizozifanya sio tu alipokuwa Rais, tangu aanze kufanya kazi. Wamezitazama hizo kwa pamoja, wakazikusanya, wakazipima kwa vigezo walivyoweka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwamba katika vigezo hivi Mheshimiwa Rais tunaweza tukamtunuku Digrii ya Falsafa hiyo ambayo amepewa. *(Makofi)*

Sasa tutafika ambapo wale wanaopewa kwa heshima wanayostahili hawana tofauti na hawa wanaolipa pesa ili wapewe hizo *degree*. *(Makofi)*

Sisi kama Taifa lazima tufahamu utaratibu upi tunataka kwenda nao, kwa sababu tusipofanya hivyo tunajipoteza

wenyewe, tunajipoteza wenyewe, hakuna mtu anayetupoteza na sisi kama viongozi lazima tuoneshe mfano. Mtoto wako umempeleka shule ili some atie bidii, leo wewe kama mzazi unalipa pesa ili upewe *degree* ya heshima unampa mfano gani yule kijana aliyeko shule unaye mkazania kusoma? Kwamba na wewe tafuta pesa, ukishatafuta pesa kalipe na wewe utapewa *degree* ya heshima. Umemtuma mtoto shule kufanya nini? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hili ninalisema kwa jumla halina uhusiana na wale waliopewa na wala haina uhusiano na kwamba wanalipa. Lakini Mheshimiwa Waziri wakati akieleza hapa sikutaka kuuliza maswali ameweka tofauti ya chuo kinachotambuliwa na chuo kisichotambuliwa. Vyuo vinavyotambuliwa duniani huwa havitoi *degree* kila wiki, kila mwezi, kila siku, kila mwaka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mimi sio kazi yangu mimi kuwaeleza ninyi, lakini kafuatilieni Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam kimeshawapa wangapi *degree* za heshima? Chuo Kikuu cha Dodoma kimeshawapa wangapi *degree* za heshima? Maana sio kwamba vyuo vya nje tu ndio vitumwagie *degree* tu za malipo, halafu vya kwetu hapa havioni mchango wetu. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu sana, ni muhimu sana kwanza sisi kama viongozi, pili sisi kama Taifa kuweka mwongozo mzuri kwa ajili ya wanaotufuata nyuma na mwongozo huo tutauweka vizuri tukifahamu Tanzania sio Kijiji, sisi ni sehemu ya dunia nzima, huko vinakotoka hivi vyuo wangeanza na nchi zao kugawia kila mtu *degree*. *(Makofi)*

Sasa nimesema hapa itafika mahali humu ndani…, nilishawahi kupata ujumbe lakini leo ngoja nimhifadhi, yuko daktari mmoja wa kisomo humu ndani alisema tunakoelekea nadhani mimi nitaandika barua niache kutambuliwa kama

daktari, kwa sababu hana tofauti yeye na huyu mwingine aliyelipa dola 2500 kulipia kile cheti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lazima tuoneshe mfano mzuri na mimi hayo nasema kwamba sisi kama Taifa hata kama maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanasema kama hawajaombwa kwamba hebu tafuteni hii *degree* ni ya namna gani, uhalisia sisi wote tunaufahamu. Namna *degree* za heshima zinavyotolea tunaufahamu, hizi nyingine zinazoleta wageni kwa ajili ya kuleta makablasha ya vyeti vya kugawia watu wakiuza kama pipi haikubaliki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunajivunjia heshima kama Taifa hasa kwenye eneo letu la elimu, lakini pia kwenye eneo la kuwapa heshima wanaostahili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo na kwa sababu msimamizi wa sekta yuko hapa na amesema, haya niliyoyasema hayawazuii kuendelea na utaratibu wenu, lakini mchukue jukumu la kufanya kama viongozi ambao kuna watu wanawatazama nyuma na ninyi mna watoto wako shule na mngependa wasome, wasome mpaka wakutane na kibao kimegeuka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo nahairisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 5:35 Asubuhi Bunge lilihairishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 10 Februari, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*